
Nipashe
Jumamosi Julai 27, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0579981
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



## Wanakijiji wawafikisha polisi wauguzi tuhuma za wizi dawa

UKURASA 4




UKURASA 13

# JPM afichua upigaji wa kutisha Selous

• **Hoteli** ya kitalii yatoza mil. 7/- kwa siku, atilia shaka mgawo, kodi kwa serikali, CAG Assad ataja kiini cha tatizo... *Endelea ukurasa 2*



Rais John Magufuli akiangalia michoro ya ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa Megawati 2115, eneo la Mto Rufiji, katikati ya mikoa ya Morogoro na Pwani, baada ya kuweka jiwe la msingi la mradi huo, jana. Kushoto ni Waziri wa Nishati wa Misri, Dk. Mohamed Shaker. **PICHA: IKULU**

## Ushahidi wa video waibua mvutano

UKURASA 3

## Chadema yamjibu kigogo CCM mchezo chandimu

UK.2

**MICHEZO** **AUSSEMS: WATASUBIRI** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# JPM afichua upigaji wa kutisha Selous

**Na Waandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amefichua upigaji wa mabilioni ya shilingi kwenye Pori la Akiba la Selous huku akitilia shaka kama serikali inaambulia chochote kupitia kodi mbalimbali.

Pia ametaja sababu za kupigwa vita kwa mradi wa uzalishaji umeme wa maji katika Mto Rufiji, maarufu kama Stiegler's Gorge.

Rais Magufuli aliyasema hayo jana wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi wa bwawa la mradi huo unaotarajiwa kugharamu Sh. trilioni 6.5 (fedha za ndani) kwa lengo la kuzalisha MW 2,115.

Alisema mradi huo kwa muda mrefu umeshindwa kutekelezwa kutoka na kupigwa vita kutoka ndani na nje ya nchi ili serikali iendelee kuuziwa umeme kwa gharama kubwa, lakini ameamua kutekeleza sasa kwa kuwa anaamini kwenye nyuki wakali kuna asali.

Kiongozi huyo wa nchi alibainisha kuwa katika eneo hilo kuna mradi wa hoteli na nyumba ambazo hana hakika kama serikali inaambulia mgawo wowote na kama maofisa usalama wanafahamu mali zinazosafirishwa kutoka eneo hilo.

"Leo (juzi) nimelala kule na niliamua kuja kulala hapa. Kule kuna hoteli chumba kimoja ni Dola za Marekani 3,000 (Sh. milioni 6.885), Watanzania wengi hamjui, lakini kuna nyumba na hoteli kule ni nyingi.

"Chumba kimoja Dola 3,000 na watu wanalipa, wanakuja na ndege wanapaki wanalala, wakishamaliza wanaondoka na ndege wanaenda Ulaya," alisema.

Aliongeza kuwa hana uhakika kama Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Khamis Kigwangalla, anafahamu asilimia ngapi ya fedha zinazokusanywa kupitia miradi hiyo na kama vyombo vya ulinzi na usalama vinafahamu ni mali kiasi gani zinasafirishwa kutoka katika eneo hilo.

"Hiyo ndiyo Tanzania. Ukiona unaenda eneo fulani, ukakuta nyuki wa pale ni wakali sana, wanakuvamia wakitaka kukuuma, ujue kuna asali.

"Watanzania wote wanafahamu ukienda sehemu ambayo kuna nyuki na hawahangaiki na wewe ujue asali haipo. Lakini ukiona kuna nyuki wanakuvamia wanataka

INAENDELEA UK. 8



Mjasiriamali akionja chachandu anayotengeneza kabla ya kuijaza kwenye chupa, kwa ajili ya kuwauzia wateja wake, katika eneo la Feri, Magogoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Chadema wamjibu kigogo CCM mchezo wa chandimu

**Na Romana Mallya**

SIKU chache baada ya Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, kudai upinzani unapenda kushadadia mambo ya kitoto, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimemjibu kigogo huyo.

Katika majibu yake kwa Dk. Bashiru, chama hicho kikuu cha upinzani nchini, kimemtaka mtaalamu huyo wa sayansi ya siasa atafute mbinu za kuinusuru CCM ambayo kimedai inakaribia kufa kutokana na migogoro.

Mapema wiki hii, akiwa mkoani Dodoma, Dk. Bashiru akizungumzia sakata la malumbano yaliyokuwa yakiendelea ndani ya CCM, alisema huo ni mchezo wa kitoto ndiyo maana wapinzani wameanza kuuchangamkia.

Ofisa Habari wa Chadema, akizungumza na Nipashe jana, alimtaka kigogo huyo wa CCM ashughulike na watu wa chama chake (CCM) kwa kuwa chama hicho tawala kinaelekea kufia mikononi mwake.

"Ni vizuri Bashiru ashughulike na chama chake kinachotaka kumfia kabla ya kuhangaika na wapinzani, chama kinawafia, wanatafuta ahueni upinzani, wanalumbana wenyewe, wanatutaja upinzani, apambane na CCM yake inayokufa," alisema Makene.

Akiwa Dodoma mwanzoni mwa wiki, Dk. Bashiru alisema: "Wao wanacheza chandimu, sisi tupo ngazi ya juu, 'game' (mchezo) yetu ni ya viwango vya kimataifa, ukiona wapinzani wamechangamkia porojo na upuuzi ndani ya CCM, ujue hao walioanzisha hawakitakii mema chama chetu na hawajui vizuri taratibu za chama.

"Mchezo wa kitoto waachiwe

INAENDELEA UK. 8

# Mwandishi mkongwe Kabigi afariki dunia

**Na Mwandishi Wetu**



JUMUIYA ya wanahabari nchini imeondokewa na mwanahabari mbobezi Agnes Kabigi (53), aliyefariki dunia ghafla jana mchana, akiwa kazini Kahama mkoani Shinyanga.

Taarifa za kifo cha Agnes zilizosambaa jana mchana kwenye mitandao ya kijamii, zilithibitishwa na Mkurugenzi wa Shirika la Kimataifa la AGPAHI, Dk. Sekele Mwakyusa, alilokuwa akifanya kazi.

Akizungumza na Nipashe jana jijini Dar es Salaam, Dk. Mwakyusa alisema Kabigi alifariki dunia akiwa amekaa kwenye kiti ndani ya gari la ofisi.

Alisema Kabigi na wenzake kuanzia juzi walikuwa Shinyanga kwa shughuli za kikazi, ikiwamo kutembelea sehemu na wadau wa AGPAHI, inayoshughulika na masuala ya kudhibiti virusi vya Ukimwi (VVU) na Ukimwi inakofanya kazi.

Kwa mujibu wa Dk. Mwakyusa Kabigi aliwasili Kahama juzi na kueleza kuwa alikuwa akijisikia vibaya, lakini hali haikuwa mbaya, hivyo hakwenda hospitalini.

Dk. Mwakyusa alisema pamoja na hali yake kiafya, aliendelea na kazi na kwamba hadi jana asubuhi hakuwa na tatizo na aliondoka na wenzake kwenda kwenye kazi wakipitia Hospitali ya Wilaya ya Kahama kwa ajili ya kuchukua nyaraka walizokuwa wanazihitaji.

Ofisa huyo alisema baada ya kuwasili kwenye hospitali hiyo, mwenzake alishuka kuzifuata na kumwacha Agnes akiwa amekaa kwenye gari hilo na aliporejea alikuta amefariki dunia na kukimbizwa hospitalini ambako ilithibitika amekutwa na umauti.

Alisema Kabigi aliyejiunga na shirika hilo akiwa Meneja wa Mawasiliano Julai, mwaka jana, mwili wake unatarajiwa kurudishwa Dar es Salaam leo kwa taratibu zaidi za mazishi.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, familia yake inatarajia kuwa mazishi yake yatafanyika keshokutwa au Jumanne wiki ijayo.

**HISTORIA**

Agness Kabigi aliyezaliwa miaka 53 iliyopita, alisoma katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Kibosho mwaka 1982 hadi 1985 na kitaaluma ni mwanahabari aliyesoma katika kilichokuwa Chuo cha Uandishi wa Habari Tanzania (TSJ).

Katika uhai wake, alifanya kazi Idara ya Habari (Maelezo) kabla ya kujiunga na lililokuwa Shirika la Magazeti ya Chama (sasa Uhuru Publications Limited) linalochapisha magazeti ya Uhuru, Mzalendo na Burudani.

Mwaka 1994 alijiunga na kampuni ya The Guardian Limited akiwa mwandishi mwandamizi wa gazeti la Nipashe ambako alifanya kazi kwa miaka kadhaa kabla ya kuhamia jarida la FEMINA Hip, lililokuwa likiandika taarifa za kuhamasisha vijana na jamii kujitambua na kujiepusha na Ukimwi.

Pia alitumikia Shirika la Kimataifa la Amref Health Africa, Kampuni ya Deloite akiwa Meneja Uhusiano na Mawasiliano na baadaye alijiunga na Shirika la AGPAHI.

Baadhi ya wafanyakazi wa The Guardian Ltd na Uhuru Publications alikofanyakazi miaka ya 1990 walisema alikuwa mchangamfu na mtu wa kujichanganya na wengi.

Aidha, anasifiwa kwa kuipenda fani yake ya habari na alikuwa tegemeo kwa vijana waliochipukia kutokana na kuwafunda mbinu mbalimbali za kazi na ujasiri kwenye uandishi wa habari.

**Bwana alitoa, Bwana ametwaa jina lake lihimidiwe. Amina.**



Mafundi wakichora alama za barabarani kwenye njia panda ya Maramba Mawili katika eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Ushahidi wa video wazua mvutano kesi kina Mbowe

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa utetezi katika kesi ya uchochezi inayowakabili vigogo tisa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), akiwamo Mwenyekiti wa Taifa, Freeman Mbowe, umepinga mahakama kuonyesha kumbukumbu za video ya siku ya tukio.

Aidha, upande huo umeiomba mahakama kuendelea na eneo lingine la ushahidi kwamba suala la kuonyeshwa video hiyo ni jukumu la Jamhuri na si mahakama.

Hoja hizo zilitolewa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na jopo la Mawakili wa Serikali Wakuu, Faraja Nchimbi, Paul Kadushi, Dk. Zainabu Mango, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon na Wakili wa Serikali, Salimu Msemo wakati upande wa utetezi uliongozwa na jopo la mawakili Profesa Abdallah Safari, Peter Kibatala, John Mallya na Hekima Mwasipu.

Kadushi alidai kuwa kesi imepangwa kwa ajili ya kusikilizwa na kwamba mahakama pekee ina uwezo wa kuwezesha kuonyesha kumbukumbu za kielelezo namba nne na tano (kamera na tepurekoda) kwa njia ya runinga au projekta.

Hata hivyo, Kibatala alidai kuwa upande wa Jamhuri ni jukumu lao kuandaa mazingira ikiwamo kuvitoa kama kielelezo vitendea kazi vyote.

Alidai kuwa utetezi unapinga chochote kuingia kuongezwa mbali na kielelezo namba nne na tano kama vilivyo.

Akijibu hoja za utetezi, Kadushi alidai kuwa hoja za utetezi si hoja za kisheria za kuitwa pingamizi la awali na kwamba huduma zote zinatakiwa kuandaliwa na kutolewa na mahakama yenye mamlaka hiyo.

Aliomba mahakama kuuwezesha upande wa Jamhuri kielelezo namba nne na tano kuonyeshwa mbele ya mahakama hiyo.

Hakimu alisema amesikia hoja za pande zote mbili na atatoa uamuzi Agosti 5 na itasikilizwa ushahidi wa Jamhuri mfululizo Agosti 6 na 7, mwaka huu.

Mapema mahakamani hapo, shahidi wa sita, Koplo Charles wa Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, alidai kuwa alikimbilia kwenye gari la jeshi hilo kunusuru kamera yake ya video.

Aidha, alidai kuwa mihemko ya kisiasa ilisababishwa na hamasa aliyoitoa Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, kutoa kauli ya kuwapandikiza chuki wafuasi hao dhidi ya

INAENDELEA UK. 8

# Bashiru awasha taa nyekundu kwa Sugu

**Na Augusta Njoji,** CHAMWINO

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, ametoa salamu kwa vyama vya upinzani katika uchaguzi ujao wa serikali za mitaa na Uchaguzi Mkuu.

Kiongozi huyo wa CCM pia ameonyesha wazi kuwa chama chake hakipendezwi kuona Jimbo la Mbeya Mjini likiwa chini ya mbunge wa upinzani huku akimtaka Mbunge wake, Joseph Mbilinyi 'Sugu' (Chadema) "kukaa mkao wa kula kwa kuwa hakuna uchawi wala wizi katika matokeo ambayo CCM inayapata".

Alitoa kauli hiyo juzi katika Kijiji cha Nzali wilayani Chamwino mkoani Dodoma alipozindua Ofisi ya CCM.

Alisema mtihani wa kwanza unaowakabili wapinzani kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwakani ni uchaguzi wa serikali za mitaa uliopangwa kufanyika.

"Badala ya kukesha wakijiandaa na mtihani wao wanakesha kwenye mitandao tu, waacheni walale fofofo tupige 100 kwa 100, halafu mtasikia wanasema aaah wameiba, aaah wameiba mtihani, mwalimu kawapendelea," Bashiru alisema.

Alitamba kuwa ameshajaribu mitambo na ameona ushindi upo mbele yao, akidai wapinzani watachapwa kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.

"Wanaotaka kuijua CCM mpya wajiandae kuiona na Dodoma ndiyo mliongoza mwaka 2015 kwa Tanzania Bara, sasa nawashindanisha na majiji ya Arusha, Mbeya, Mwanza, Dar es Salaam.

"Dar es Salaam nitashafanya ziara na Agosti, naenda kuwaambia nyie mlikuwa mkiani 2015, sasa mtaisoma namba, Dodoma wapo tayari 'nimeshatest' (wameshajaribu) mitambo na inafanya kazi, nimesema hivyo hivyo Arusha,"alisema.

"Na kule Arusha kuna uwezekano Halmashauri ya Karatu tukaichukua kwa sababu kuna idadi kubwa ya madiwani, Monduli, Longido, Simanjiro, Babati Mjini, Serengeti, Ukerewe, Liwale, Ukonga, Temeke, Kinondoni, Siha, Arumeru na Singida Mashariki zimerudi CCM."

Katibu Mkuu huyo aliongeza kuwa zaidi ya kata 260 zimesharudi CCM na wako tayari kwa mashambulizi kwa kuwa mitambo imeshajaribiwa.

"Natuma ujumbe kwa majiji sita, Dodoma na Arusha sina shaka, Mwanza naenda wiki ijayo 'ku-test' mitambo, nikitoka huko, naenda Tanga 'kutest' mitambo, halafu nitafunga mitambo ya mwisho kwenye majiji ya Mbeya na Bwana Sugu kaa mkao wa kula, nakuja kwako hakuna uchawi, kuna kazi," Bashiru alitamba.

Alisema ushindi wa CCM hauna wizi wala kupendelewa, hivyo wapinzani waache

INAENDELEA UK. 8

# Mwili wa mvuvi mmoja wapatikana

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

MWILI wa mvuvi mmoja aliyekufa maji baada ya mtumbwi wao wa kutumia kasia waliokuwa wanavulia dagaa kugongwa na maharamia katika Ziwa Victoria, eneo la kisiwa cha Nafuba, wilayani Bunda mkoani Mara, umepatikana na kuopolewa.

Kwa mujibu wa diwani wa Nansimo, Sabatho Mafwimbo, wananchi wa kata hiyo bado wanaendelea kutafuta mwili wa mvuvi mwingine mmoja.

Mafwimbo alisema mwili wa mvuvi uliopatikana na kuopolewa juzi ni wa Deogratus Vumilia (28), mkazi wa kijiji cha Nambaza, Bunda na kwamba mwili wa mvuvi mwingine Makongoro Makunja (48), mkazi wa kijiji hicho bado haujapatikana na juhudi za kuutafuta zinaendelea.

"Jana (juzi) tulifanikiwa kupata mwili wa mvuvi mmoja, Deogratus Vumilia, na tukauzika baada ya daktari kuufanyia uchunguzi" alisema Mafwimbo.

Alisema baada ya mwili wa mvuvi huyo kupatikana, ulifanyiwa uchunguzi na mganga mkuu wa zahanati ya Nansimo mbele ya polisi na kisha ukafanyiwa mazishi kijijini hapo.

Wavuvi hao waliokuwa watano wakiwa wanavua dagaa nyakati za usiku, mtumbwi wao uligongwa na maharamia waliokuwa na mtumbwi unaotumia mashine ya injini na kuzamishwa majini, kisha maharamia hao wakachukua zana yao aina ya kokolo la dagaa na kutokomea nazo.

Baada ya wavuvi hao kuzamishwa majini, watatu kati yao waliogelea na baadaye kuokolewa na wavuvi wenzao waliokuwa karibu na eneo hilo.

Tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia Jumanne wiki hii na baadaye wananchi waliwakamata watuhumiwa hao katika kijiji cha Kibara wilayani hapa wakiwa na kokolo walilopora ndani ya mtumbwi uliohusika kufanya unyama huo.

Polisi walisema wavuvi walionusurika kifo katika tukio hilo baada ya kuokolewa na wavuvi wenzao ni Majura Malima (18) na Siri Kabuya (16), ambao wote ni wakazi wa kijiji cha Nambaza, na Mwenda Isack (28) mkazi wa kijiji cha Kisorya wilayani Bunda.

Kutokana na tukio hilo, wananchi wenye hasira waliteketeza kwa mto mitumbwi miwili ya watuhumiwa hao pamoja ni mashine moja ya injini.

Polisi wilayani Bunda walithibitisha kuwapo kwa tukio hilo na kwamba watu kadhaa wanashikiliwa na jeshi hilo kuhusiana na uhalifu huo na kwamba upelelezi ukikamilika watawafikisha mahakamani.

HABARI KITAIFA

## Gari la polisi lapinduka na kuua askari watatu

**Na Romana Mallya**

ASKARI watatu wa Jeshi la Polisi wamefariki dunia na wengine wawili kujeruhiwa baada ya gari walilokuwa wakisafiria kupasuka tairi na kupinduka mkoani Pwani.

Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime, alisema jana kuwa ajali hiyo ilitokea juzi saa 7:30 mchana katika Kijiji cha Kilimahewa wilayani Mkuranga.

Misime aliwataja waliofariki dunia kuwa ni Ofisa Mnadhimu Mkoa wa Kipolisi Rufiji, Kamishna Msaidizi wa Polisi Issa Bukuku, Inspekta Esteria wa Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Kipolisi Rufiji na askari namba G. 1132 Pc Ibrahim wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) mkoani humo.

Alisema katika ajali hiyo, waliojeruhiwa ni dereva wa gari hilo ambaye ni F 7167 PC Ibrahim wa Ofisi ya RCO na G 7651 PC Mgusi wa Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Rufiji walilazwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH).

"Jeshi la Polisi linatoa pole kwa familia zilizopoteza wapendwa wao na marafiki zao," alisema.

Alibainisha kuwa chanzo cha ajali hiyo ni kupasuka kwa gurudumu la nyuma upande wa kulia, kulikosababisha gari kupinduka na kusababisha vifo na majeruhi. "Ajali ilihusisha gari PT. 3822 Toyota Land Cruiser mali ya Jeshi la Polisi Rufiji, lilikuwa likiendeshwa na askari mwenye namba F 7167 PC Ibrahim likitokea Ikwiriri kuelekea Kijiji cha Mwalusembe wilayani Mkuranga," alisema.



Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Kisukuru, Almano Mdede, akizungumza na wanachama wa chama hicho wa Tawi la Chemchem, akiwa katika ziara ya kusikiliza shida na kero za wananchi, katika kutekeleza agizo la viongozi wa kitaifa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MUHIDINI MSAMBA**

# JPM aagiza Selous kuwa hifadhi

**Na Mary Geofrey**

RAIS John Magufuli ameagiza mamlaka zinazohusika zihakikishe Pori la Akiba la Selous lililoanzishwa na Wajerumani mwaka 1905, ligawanywe ili kuwa na hifadhi nyingine ya taifa.

Alitoa agizo hilo jana wakati wa hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi katika mradi wa ujenzi wa bwawa la kufua umeme kwenye Mto Rufiji mkoani Pwani, maarufu Stiegler's Gorge.

Mradi huo unaotarajiwa kugharimu Sh. trilioni 6.5 kwa lengo la kuzalisha umeme MW 2,115, unatekelezwa kwa fedha za ndani.

Rais Magufuli alisema ilikuwa ni ndoto ya Rais wa Kwanza wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, kugeuza pori hilo la akiba kuwa hifadhi ya taifa na utekelezaji wake ulicheleweshwa.

Katika kutimiza ndoto hizo za Baba wa Taifa, Rais Magufuli alisema bwawa linalojengwa na hifadhi ya taifa itakayoanzishwa, vitapewa jina la Mwalimu Nyerere ili kumuenzi.

"Kwa hiyo, kwa ujumla nataka niwaeleze hii 'game reserve' haitupi faida, siku za nyuma tulikuwa tunapata 'almost' sifuri. Sasa, kutokana na hii hali na ninashukuru Waziri

INAENDELEA UK. 8




# Wanakijiji wawafikisha polisi wauguzi tuhuma wizi wa dawa

**Na Mgreth Magoso,** KIGOMA

WANANCHI wa Kijiji cha Kigogwe wilayani Buhigwe wamewafikisha katika Kituo cha Polisi Mnanila wilayani humo wauguzi wawili wa Zahanati ya Kigogwe, wakiwatuhumu kuwauzia wamiliki binafsi wa maduka ya dawa muhimu, dawa mbalimbali za zahanati hiyo zenye thamani ya zaidi ya Sh. 900,000.

Miongoni mwa dawa na vifaa tiba ambavyo wauguzi hao wanadaiwa kuviuza kwa wamiliki wa maduka ya dawa ni kipimo cha haraka cha malaria (MRDT).

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Habibu Bitwaye, jana aliwataja wauguzi waliofikishwa polisi kutokana na tuhuma hizo kuwa ni Elisante Ernest na Ndikumana Papu.

"Serikali inawajibika kuondoa changamoto ya ukosefu wa dawa lakini kuna watumishi wanatuibia wananchi kwa maslahi yao binafsi, leo ni arobaini yao.

"Wapo kituo cha polisi kwa kosa la kuiba dawa mbalimbali hasa vipimo vya ugonjwa wa malaria, dawa ya mseto na amoxilin zenye thamani ya zaidi ya Sh. 900,000, tumebaini kuwa huwauzia wamiliki binafsi wa maduka ya dawa," alidai.

Alidai kuwa katika harakati za kukamata watuhumiwa, mmoja wa wanunuzi wa dawa hizo alifanikiwa kutoroka, lakini baadaye alijisalimisha polisi baada ya mke wake kukamatwa.

Bitwaye aliwapongeza wananchi wake kwa kushiriki kuwafichua wahalifu wa mali za umma, huku akiikumbusha Serikali Kuu kufanya ukaguzi ili kuwabaini watumishi wasio waadilifu wanaohatarisha maisha ya Watanzania kwa kukosa dawa katika zahanati.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Paul Chaote, alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia suala hilo, alikiri kupokea taarifa za kukamatwa kwa watendaji wake na kuwataka watumishi wote wa umma kuzingatia miiko ya kazi na kutii sheria za utumishi.

**TANGAZO**

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
# PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
# TARIME DISTRICT COUNCIL

## CONSOLIDATED STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30th JUNE, 2018

| | Notes | 2018 TZS | 2017 TZS |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| **Current assets** | | | |
| Cash at Bank | 24 | 4,539,820,632 | 2,886,207,932 |
| Receivables | 25 | 16,624,385 | 209,591,000 |
| Inventories | 26 | 349,176,358 | 206,244,495 |
| | | **4,905,621,375** | **3,302,043,427** |
| **Non-current assets** | | | |
| Property, plant and equipment | 29 | 89,637,817,829 | 90,959,083,317 |
| Forestry assets | 32 | 188,125,875 | 188,125,875 |
| Other financial assets | 27 | 28,433,700 | 28,433,700 |
| Investment | 45 | - | - |
| | | **89,854,377,404** | **91,175,642,892** |
| **TOTAL ASSETS** | | **94,759,998,778** | **94,477,686,318** |
| **LIABILITIES** | | | |
| **Current liabilities** | | | |
| Payables | 35 | 2,939,781,232 | 2,247,703,852 |
| Deferred income Recurrent | 11 | 933,912,135 | 1,449,938,652 |
| | | **3,873,693,367** | **3,697,642,504** |
| **Non-current liabilities** | | | |
| Deferred income (Capital Grant) | 41 | 8,925,167,319 | 9,388,931,863 |
| Reserves - MCR | 27 | 27,371,743 | 14,216,850 |
| | | **8,952,539,062** | **9,403,148,713** |
| **TOTAL LIABILITIES** | | **12,826,232,429** | **13,100,791,218** |
| **TOTAL NET ASSETS** | | **81,933,766,349** | **81,376,895,100** |
| **NET ASSETS** | | | |
| Accumulated surplus/(deficit) | | **81,933,766,349** | **81,376,895,101** |
| **TOTAL NET ASSETS** | | **81,933,766,349** | **81,376,895,102** |

The notes on pages 21 to 58 form part of these financial statements.

These financial statements were authorised by the full council Meeting for issue on 26.09.2018 and were signed on its behalf by:

Apoo Castro Tindwa
DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR TARIME DISTRICT COUNCIL

Moses Misiwa
COUNCIL CHAIRMAN
CHAIRMAN TARIME DISTRICT COUNCIL

## CONSOLIDATED STATEMENT OF FINANCIAL PERFORMANCE FOR THE YEAR ENDED 30th JUNE, 2018

| | Notes | 2018 TZS | 2017 TZS |
|---|---|---|---|
| **Revenue** | | | |
| Local taxes | 9 | 3,782,359,198 | 4,183,199,275 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 10 | 649,202,833 | 1,299,031,098 |
| Amortisation of recurrent grants | 11 | 25,093,843,888 | 23,647,926,501 |
| Amortisation of capital grant | 41 | 1,050,855,285 | 2,855,345,906 |
| Other own source revenue | 16 | 2,750,394,555 | - |
| **Total Revenue** | | **33,326,655,759** | **31,985,502,780** |
| **Expenses** | | | |
| Wages, salaries and employee benefits | 17 | 22,175,083,828 | 21,737,016,841 |
| Supplies and consumables used | 18 | 1,651,244,259 | 1,147,786,909 |
| Maintenance expenses | 19 | 806,943,052 | 1,857,834,007 |
| Grants and other transfer payments | 20 | 5,071,672,083 | 2,543,997,571 |
| Depreciation of property, plant and equipment | 29 | 3,064,841,288 | 2,855,345,906 |
| **Total Expenses** | | **32,769,784,510** | **30,141,981,233** |
| **Surplus/(deficit) during the year** | | **556,871,249** | **1,843,521,547** |

The notes on pages 21 to 58 form part of these financial statements.

These financial statements were authorised by the full council Meeting for issue on 26.09.2018 and were signed on its behalf by:

Apoo Castro Tindwa
DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR TARIME DISTRICT COUNCIL

Moses Misiwa
COUNCIL CHAIRMAN
CHAIRMAN TARIME DISTRICT COUNCIL

## CONSOLIDATED CASH FLOW STATEMENT FOR THE YEAR ENDED 30th JUNE, 2018

| | Note | 2018 TZS | 2017 TZS |
|---|---|---|---|
| **Cash flows from operating activities** | | | |
| **Receipts** | | | |
| Local taxes | 9 | 3,782,359,198 | 4,183,199,275 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 55 | 842,169,448 | 1,299,031,098 |
| Other own source revenue | 16 | 2,750,394,555 | - |
| Recurrent grants | 55 | 24,148,439,491 | 23,550,251,805 |
| | | **31,523,362,693** | **29,032,482,178** |
| **Payments** | | | |
| Wages, salaries and employee benefits | 55 | (21,689,363,120) | (21,000,102,562) |
| Supplies and consumables used | 55 | (1,157,641,571) | (990,760,050) |
| Maintenance expenses | 19 | (806,943,052) | (1,857,834,007) |
| Grants and other transfer payments | 55 | (5,059,317,190) | (2,543,997,571) |
| | | **(28,713,264,933)** | **(26,392,694,191)** |
| **Net cash from operating activities** | | **2,810,097,760** | **2,639,787,987** |
| **Cash flows from investing activities** | | | |
| Purchase of property, plant and equipment | 29 | (2,018,984,788) | (2,102,910,686) |
| Proceeds for Purchase of PPE | 45 | 862,499,730 | 183,527,248 |
| **Net cash from investing activities** | | **(1,156,485,058)** | **(1,919,383,438)** |
| **Cash flows from financing activities** | | | |
| Development Grants Received | 28 | - | - |
| **Net cash used in financing activities** | | **-** | **-** |
| **Net increase in cash at bank** | | 1,653,612,702 | 720,404,551 |
| Cash at bank at beginning of period | | 2,886,207,932 | 2,165,803,382 |
| **Cash at bank at end of period** | | **4,539,820,632** | **2,886,207,932** |

**The notes on pages 21 to 58 form part of these financial statements.**

These financial statements were authorised by the full council Meeting for issue on 26.09.2018 and were signed on its behalf by:

Apoo Castro Tindwa
DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR TARIME DISTRICT COUNCIL

Moses Misiwa
COUNCIL CHAIRMAN
CHAIRMAN TARIME DISTRICT COUNCIL

**Unqualified Opinion**

I have audited the financial statements of Tarime District Council, which comprise the Statement of Financial Position as at 30th June, 2018, and the Statement of Financial Performance, Statement of Change in Equity and Statement of Cash Flows for the year then ended, and notes to the financial statements, including a summary of Significant Accounting Policies.

In my opinion, the accompanying financial statements of the Tarime District Council are prepared in all material respects, in accordance with International Public Sector Accounting Standards (IPSAS) Accrual basis of accounting and in the manner required by the Public Finance Act, 2001 revised 2004/Local Government Finances Act 1982, revised 2000.

**Report on Other Legal and Regulatory Requirements**

**Compliance with the Public Procurement Act, 2011**

In view of my responsibility on the procurement legislation and taking into consideration the procurement transactions and processes I have reviewed as part of this audit, I state that, Tarime District Council procurement transactions and processes have generally complied with the requirements of the Public Procurement Act No. 7 of 2011 and its underlying Regulations of 2013.

Prof. Mussa Juma Assad,
Controller and Auditor General
31st March, 2019

National Audit Office of Tanzania,
P.O. Box 950,
11101 Dodoma, Tanzania.
Tel: 255 (026) 2321759
Fax: 255 (026) 2117527
Email: ocag@nao.go.tz

215343702

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Kila la kheri Stars michuano ya CHAN

**KUMALIZIKA** kwa safari moja, ndio mwanzo wa safari nyingine. Hayo ndiyo maisha ya soka yalivyo.

Julai 19 mwaka huu, jijini Cairo nchini Misri, kulifanyika fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon 2019), na kikosi cha Algeria, kilifanikiwa kutangazwa kuwa wafalme wapya wa mashindano hayo.

Algeria ilichukua ubingwa huo baada ya kuwafunga Senegal bao 1-0, na kombe hilo kuwa ni la pili kwa nchi yao kulibeba katika michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Baada ya kumalizika kwa michuano hiyo ya Afcon, ambayo huchezwa kila baada ya miaka miwili, tayari CAF imeshafungua kalenda mpya ya mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Mashindano hayo ya CHAN yalianza kuchezwa mwaka 2008, na Taifa Stars ambayo wakati huo ilikuwa chini ya Kocha Mkuu Mbrazil Marcio Maximo, ilifanikiwa kushiriki michuano hiyo iliyochezwa nchini Ivory Coast, nahodha akiwa ni Nadir Haroub "Cannavaro".

Katika safari hii ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za CHAN, timu ya Tanzania (Taifa Stars), itaanza kampeni yake kesho kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam kwa kuwakaribisha majirani zake Kenya (Harambee Stars).

Ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kusonga mbele katika mashindano hayo, Taifa Stars inahitaji ushindi mnono ili kurahisisha kazi kwenye mechi ya marudiano ambayo itachezwa baada ya wiki moja huko jijini Nairobi.

Stars inahitaji kupata ushirikiano kutoka kwa wadau mbalimbali ambao watakuwa nayo karibu kama walivyofanya katika mchezo wa mwisho wa kuwania tiketi ya kushiriki fainali zilizopita za Afcon, ambapo ilicheza dhidi ya Uganda (The Cranes). Ushirikiano, umoja na nguvu ulizotumika katika kuhakikisha Taifa Stars, inashinda mechi ile, ni vema ukaendelea katika kuhakikisha kesho Harambee Stars inafungwa na kuwapa matumaini mapya ya kusonga mbele na kufuzu michuano hiyo kwa mara ya pili.

Kama ilivyokuwa katika fainali za Afcon, wachezaji wanatakiwa kujituma katika mechi zote watakazocheza, kwa sababu ni nafasi yao nyingine ya kutangaza vipaji vyao kwa mawakala mbalimbali wanaosaka wachezaji bora kutoka katika nchi za Afrika. Kwenye soka hakuna miujiza. Kila Mtanzania anatakiwa kutekeleza majukumu yake ili kuhakikisha timu hiyo inapata matokeo mazuri katika mchezo huo wa kwanza na ule wa marudiano na hatimaye kusonga mbele.

Nipashe linaamini kuwa, ili ndoto za kucheza fainali hizo kwa mara ya pili ziweze kutimia, wachezaji pia wanatakiwa kujituma kuanzia mazoezini hadi uwanjani kwa wale watakaopata nafasi ya kupangwa. Ushirikiano kati ya wachezaji wa timu hiyo ni jambo lingine muhimu linalotakiwa kuonekana kwa sababu inaongeza kujenga morali na hamasa.

Katika kuhakikisha mambo yanakwenda vema, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), lilimteua Mrundi Etienne Ndayiragije kuiongoza timu hiyo kwa muda kwa kushirikiana na Wazalendo, Juma Mgunda na Suleiman Matola.


Huu ni wakati mwingine pia wa wadau wa michezo nchini na serikali kuwapa ushirikiano makocha hawa ili waweze kutimiza malengo ya kufuzu michuano hiyo kama ilivyokuwa kwa walimu wengine waliopita.

Tunasema kuwa, wachezaji wakijituma na wakipambana, hakuna kitakachoshindikana, Stars itapata ushindi na kwenda Nairobi ikiwa na nguvu na si kuwafuata wapinzani wao kwa ajili ya kukamilisha ratiba.

Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Taifa Stars.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

## Cha wenyewe huliwa na wenyewe

**KITU** cha watu wengine huwafaidi wao wenyewe. Methali hii yaweza kutumiwa kuwahimiza watu wajitegemee.

Husemwa "Chako ni chako, cha mwenzako si chako." Maana yake kitu unachokiita chako ni kizuri na huweza kukufaa; tena una uhuru nacho kuliko cha mtu mwingine.

"Mtaka cha mvunguni sharti ainame." Maana yake anayekitaka kitu kilicho mvunguni mwa kitanda, lazima ainame ndipo aweze kukichukua. Methali hii hutumiwa kutukumbusha kwamba tunapokitaka kitu fulani lazima tuwe tayari kukifanyia kazi au kukisumbukia.

Pia "Kambare mkunje angali m-bichi." Maana yake mkunje kambare akiwa m-bichi kwani anapokauka haiwezekani kumkunja.

Nchi za wenzetu huwa na wachezaji wazuri wa kandanda kuliko sisi. Wao hujiandaa kwa kuwafunza vijana wadogo. Vilabu vya huko huwa na shule maalumu za kuwafunza watoto. Wanapokomaa huvitumikia vilabu vyao au kuuzwa kwa vilabu vingine. Kuna wakati niliandika kwenye safu hii ya 'Mungwana lazima nilonge' kuwa TFF imekosea kuruhusu vilabu vya Ligi Kuu Tanzania Bara kusajili wachezaji 10 wa kigeni. Kwa kawaida timu ya kandanda huwa na wachezaji 11 uwanjani. Endapo wachezaji wote 10 wa kigeni watakuwa bora zaidi ya wenyeji, watachezeshwa wote na mmoja tu ndio mwenyeji. Tunatwanga maji kwenye kinu! Hivi karibuni, Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, alikubaliana na msimamo wa TFF kuruhusu vilabu kusajili wachezaji 10 wa kigeni!

Waziri ameweka sharti kuwa watakaosajiliwa kutoka ughaibuni ni lazima wawe wachezaji wanaoshiriki Ligi Kuu na pia timu za mataifa yao. Amesema lengo ni kudhibiti idadi kubwa ya wachezaji wa kigeni wanaosajiliwa humu nchini kumbe hawana viwango bora!

Alisema "Wallace Karia alipoingia madarakani aliongeza idadi ya kusajili wachezaji wa kigeni kutoka watano hadi 10 kwa kila klabu na suala hilo lilimsumbua sana bungeni hata kupendekeza kuwe na mjadala mpana utakaowahusisha wadau wa kandanda nchini."

"Hatutaki kila mchezaji aliyeibukia kwenye ndondo (mechi za mitaani) aje kucheza kwenye ligi yetu. Ndio maana tumeridhia wachezaji 10 wa kigeni wasajiliwe kwa masharti hayo. Mwaka jana walisajiliwa wachezaji 52 wa kigeni na mwaka huu walisajiliwa 42," alisema Dk. Mwakyembe.

Hata hivyo Rais wa Shirikisho la Kandanda Nchini (TFF), Karia amesema nchi zilizoendelea kimpira zikilinganishwa na Tanzania, wachezaji wanaocheza Ligi Daraja la Pili au la Kwanza wataangaliwa.

Baadhi ya wachezaji wa kigeni waliosajiliwa kwa fedha lukuki wameonekana si lolote wakilinganishwa na wachezaji wetu. Kama mchezaji wa kigeni hayumo kwenye timu ya taifa lake hafai. Wachezaji kama hao wanaposajiliwa watazisaidiaje timu zetu? Wangekuwa bora wangechukuliwa na timu za nje hivyo wasingeachwa kwenye timu za mataifa yao.

Nionavyo, TFF ingeweka utaratibu wa kuzuia usajili wa fujo na mbwembwe kwani wengi wanaosajiliwa kwa pupa na ushindani huishia kuwakodolea wenzao wakicheza, nao kuwa wachezaji wa akiba. Kuna wakati huwa hivyo kwa muda mrefu mpaka wengine kukata tamaa na kutaka wauzwe kwa vilabu vingine ili vipaji vyao visishuke.

Katika tukio lingine, serikali imetoa mwongozo wa mfumo wa uendeshaji wa vilabu vya kandanda vilivyoanzishwa na wananchi humu nchini. Kwamba asilimia 49 ya hisa hazipaswi kuhodhiwa na mtu mmoja bali watu watatu, huku asilimia 51 zilizosalia zibaki kwa wanachama.

Waziri Mwakyembe ameshauri iundwe kamati ndogo ya wataalamu ili kuweka kanuni vizuri. Kamati hiyo itakuwa na mjumbe mmoja mmoja kutoka BMT, TFF, Kurugenzi ya Michezo, mwakilishi wa wadau, TRA na wajumbe wawili kutoka Soko la Hisa na Mitaji.

Mbali na hayo, bado kuna mambo mengi yanayotakiwa kufanyiwa kazi. Lazima vilabu vya mpira vilazimishwe kuwa na viwanja vyao wenyewe kama zilivyo Azam, Mtibwa na Kagera Sugar. Kuwe na kanuni kuwa kila klabu ya kandanda iwe na kiwanja cha mashindano na mazoezi ikiwamo ukumbi wa michezo ya mazoezi ya viungo, bwawa la kuogolea na vituo vya afya kwa ajili ya wachezaji. Ili kutimiza jambo hili, TFF yapaswa kuonesha mfano kwa kuwa na kiwanja chake kitakachokuwa mfano kwa vilabu.

Jambo lingine la kufanyiwa kazi ni CCM kuteka viwanja vya michezo ambavyo havikujengwa na chama hicho! Viwanja vyote vinavyomilikiwa na chama hicho havifai na vinatia aibu. Kinachotambulisha viwanja vinavyomilikiwa na CCM ni rangi za njano na kijani tu, lakini havitunzwi! Huo ndio utunzaji wa viwanja?

Ushauri wangu ni viwanja hivyo kuwa mikononi mwa halmashauri za miji na majiji na fedha zitakazopatikana zitumiwe kuviboresha kwani vilivyo sasa vinatia aibu!

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# Kesi ya Dk. Tenga na wenzake yapigwa kalenda

Na Hellen Mwango

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imeahirisha kesi ya kutakatisha fedha inayowakabili vigogo wa Kampuni ya Six Telecoms akiwamo Wakili Mwandamizi wa Kujitegemea, Dk. Ringo Tenga, mpaka baada ya siku 14 itakapotajwa tena.

Kesi hiyo ilipangwa kutajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa upande wa Jamhuri bado haujakamilisha kuandaa nyaraka muhimu za kesi hiyo.

Kutokana na madai hayo, hakimu alisema kesi hiyo itatajwa Agosti 8, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu. Mapema Aprili 5, mwaka huu upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika.

"Mheshimiwa hakimu kesi hii imepangwa kwa ajili ya kutajwa na Jamhuri tunaifahamisha mahakama kwamba upelelezi wake umekamilika tunaandaa nyaraka kwa ajili ya kuanza mchakato wa kusikilizwa," ulidai upande wa Jamhuri.

Mbali na Dk. Tenga washtakiwa wengine ni Mhandisi na Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Hafidhi Shamte maarufu Rashidi Shamte, mfanyabiashara na mkurugenzi wa kampuni hiyo, Peter Noni, Mkuu wa Fedha wa kampuni hiyo, Noel Chacha na kampuni ya Six Telecoms Limited. Wote wanadaiwa kutakatisha Sh. bilioni nane.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka sita yakiwamo ya utakatishaji wa fedha, kuwafanya wakae mahabusu kwa kuwa makosa hayo hayana dhamana kwa mujibu wa sheria.



Mwanafunzi wa Shule ya Baobab ya Mapinga wilayani Bagamoyo, Mkoa wa Pwani, Noreen Lyimo, aliyeongoza kitaifa kwenye masomo ya biashara katika mtihani wa kidato cha sita akiwa amebebwa juu juu na wenzake baada ya kufika shuleni hapo juzi, kwa ajili ya kupongezwa na uongozi wa shule hiyo ambapo alizawadiwa kompyuta mpakato ya kisasa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Aliyeongoza kitaifa azawadiwa kompyuta

Na Mwandishi Wetu

SHULE ya Sekondari ya Baobab iliyoko Mapinga, Bagamoyo mkoani Pwani, imemzawadia kompyuta mpakato ya kisasa mwanafunzi wa shule hiyo, Noreen Lyimo, ambaye aliongoza kitaifa kwenye masomo ya biashara.

Noreen alikabidhiwa kompyuta hiyo jana shuleni hapo kwenye hafla iliyoandaliwa na shule hiyo. Mgeni rasmi alikuwa Mkuu wa Shule ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDBS), Profesa Ulingeta Mbamba.

Mgeni mwingine mashuhuri aliyehudhuria hafla hiyo ni Ofisa Elimu wa Mkoa wa Pwani, Abdul Maulid, na Mwenyekiti wa Bodi ya Shule hiyo, Bakari Bakari.

Mkuu wa shule hiyo, Venance Hongoa, alimsifu Noreen kwa namna alivyoipa sifa shule hiyo kutokana na kuwa na bidiii tangu alipoanza kidato cha kwanza shuleni hapo mwaka 2013 kwa kuwa amekuwa akishika nafasi ya kwanza.

Alisema Noreen alipata daraja la kwanza kwenye mtihani yake ya kidato cha nne na kwenye ufaulu wa kidato cha sita na amekuwa wa kwanza kitaifa amefanikiwa kupata daraja la 1.4.

"Kwa muda mrefu Noreen anajitambua sana, anajua amekuja shule kufanya nini na amekuwa mwenye nidhamu ya hali ya juu na mtu anayejali muda na anatumia fursa zinazopatikana vizuri. Naweza kusema ameyatendea haki mazingira mazuri ya hii shule," alisema.

Alisema licha ya uchanga wa shule hiyo, imekuwa ikipata mafanikio makubwa mwaka hadi mwaka na kwamba wamekuwa wakifaulisha wanafunzi wa kidato cha nne kwenda cha tano na cha sita kwenda vyuo vikuu mbalimbali kwa zaidi ya asilimia 90. Kwa upande wake, Profesa Mbamba aliwataka wanafunzi wa shule hiyo wahakikishe wanakuwa na tabia njema ili wafaulu kwa kiwango cha juu kama alivyofanya Noreen.

Alisema gharama ya ujinga ni kubwa sana kuliko kusoma hivyo aliwataka waachane kabisa na tabia za ovyo ovyo zinazoweza kuwa kikwazo kwao kufaulu kwa kiwango kilichofikiwa na mwenzao.

Naye Ofisa Elimu wa Mkoa wa Pwani, Maulid, alisema Baobab ni shule nzuri yenye mazingira bora ya kusomea na ndiyo sababu imefanikiwa kutoa mwanafunzi bora kitaifa kwenye mchepuo wa biashara.

Alisema anajisikia fahari kuona mwanafunzi bora akitokea mkoa wa Pwani na kwamba atajitahidi kuendelea kuweka mazingira bora ili wanafunzi wengi bora kitaifa watokee kwenye mkoa huo.

# Matokeo yaipa 'jeuri' shule

Na Mwandishi Wetu

SHULE ya Sekondari ya Pius iliyoko Mbagala jijini Dar es Salaam, imejivunia kupata matokeo mazuri ya kidato cha sita yaliyotangazwa na Baraza la Taifa la Mitihani (Necta) hivi karibuni.

Mkuu wa Shule huyo, Stephen Haruna, alisema jana kuwa wamefurahi kutoa wanafunzi wengi kwenda vyuo vikuu mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Alisema kwenye matokeo hayo, wametoa wanafunzi tisa wa daraja la kwanza, 19 daraja la pili na 25 wamepata daraja la tatu na hakuna daraja la nne wala sifuri.

Haruna alisema shule hiyo imekuwa na kawaida ya kuchukua wanafunzi wenye uelewa wa aina tofauti tofauti hata wale wenye uelewa mdogo na kisha huwaandaa vyema na katika mazingira mazuri kwa ajili ya mitihani ya kitaifa na mwishowe hufanya vyema.

"Walimu wamefanya kazi kubwa kuhakikisha tunapata matokeo mazuri kama haya. Tunashukuru juhudi za walimu na ushirikiano wa wazazi, uongozi wa shule na wanafunzi wenyewe. Uongozi nao umeweka mazingira wezeshi ya kujifunza na kufundisha ndiyo sababu hatujapata daraja la nne wala 0," alisema.

Alisema hata kwenye matokeo ya kidato cha pili na cha nne, wamekuwa wakifaulisha wanafunzi wengi kwa daraja la kwanza na la pili kutokana na jitihada kubwa zinazofanywa na walimu na uongozi.

"Tunawapongeza sana walimu wetu kwa namna wanavyotupa ushirikiano mkubwa kuhakikisha shule yetu inaendelea kuwa juu mwaka hadi mwaka tunawaomba waendelee kutupa ushirikiano kama huo ili Pius iendelee kuwa juu mwaka hadi mwaka," alisema.

"Kwa matokeo haya tunaomba wazazi watuamini watuletee watoto wao tuwalee hapa Pius High School kwani kuna michepuo yote, mazingira mazuri ya kusomea na nawahakikishia wazazi hawatajuta kuwaleta watoto wao maana tutahakikisha wanafaulu kwa madaraja ya juu.

Alisema kuna mambo mengi yamechangia matokeo mazuri kama hayo ikiwamo mazingira bora ya kufundishia yaliyowekwa na uongozi wa shule hiyo kwa walimu na wanafunzi ikiwamo maabara na maktaba za kisasa za shule hiyo.

# Ushahidi wa video wazua mvutano

INATOKA UK. 3

serikali.

Akiongozwa na Wakili Kadushi, shahidi alidai kuwa Februari 16, 2018 alipangiwa kazi kama mwandishi wa habari kufanya kavareji ya mkutano wa kufunga kampeni wa Chadema katika viwanja vya Buibui vilivyoko Kinondoni, Dar es Salaam.

Alidai kuwa alijiandaa na vitendea kazi vyake ikiwamo kamera ya kupiga picha za video na ilipofika saa 10 alifika katika viwanja hivyo kwa ajili ya kuanza kazi.

"Nilipofika watu walianza kukusanyika na mshereheshaji alitangaza kwamba viongozi wakuu wa chama wameshafika, baada ya muda wabunge na viongozi wakuu walipanda jukwaani nilimsikia Mbowe akitoa kauli za kufanya hamasa ya kuichukia serikali," alidai na kuongeza kuwa:

"Wanachama walipata hamasa na mihemko iliyosababisha wapate jazba ya kuichukia serikali na vyombo vya ulinzi na usalama, wananchi waliokuwa wamekaa walinyanyuka na kuhamasika, mimi na waandishi wenzangu tulitawanyika pale tuposimama karibu na jukwaa, nilikimbilia kwenye gari polisi kunusuru kamera," alidai Koplo Charles.

Mbali na Mbowe, washtakiwa wengine ni Mbunge wa Bunda Mjini, Ester Bulaya; Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko, Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vincent Mashinji; Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa; Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu: Mbunge wa Kibamba, John Mnyika; Mbunge wa Kawe, Halima Mdee na John Heche wa Tarime Vijijini.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Februari Mosi na Februari 16, mwaka jana, Mbowe na wenzake wakiwa Kinondoni, Dar es Salaam kwa pamoja walikula njama na wengine ambao hawapo mahakamani ya kutenda kosa la jinai ikiwamo kuendelea na mkusanyiko isivyo halali na kusababisha chuki na uchochezi wa uasi.

# JPM afichua upigaji wa kutisha Selous

INATOKA UK. 2

kukuuma, anza kutafuta mbinu za kupata asali," alisema.

Rais Magufuli alisema eneo hilo ni asali kwa Watanzania ndiyo sababu ya kuwapo kwa vita hiyo kubwa ya kuuzuia mradi huo ambao utazalisha umeme mwingi ambao haujawahi kuzalishwa nchini tangu Tanzania ipate uhuru miaka zaidi ya 50 iliyopita.

Alisema kiasi hicho cha umeme kitakachozalishwa ni kikubwa kuliko umeme wote unaozalishwa kwa sasa nchini ambao ni MW 1,601, hivyo kuwataka Watanzania kutembea kifua mbele.

Rais Magufuli alisema mradi huo pia utawezesha utunzaji mazingira kwa sababu eneo litakalotumika ni chini ya asilimia tatu ya hekta 50,000 zilizopo na bwawa litakalochimbwa litatumika kwa ajili ya uvuvi na shughuli za utalii.

"Suala la uhifadhi mazingira hatuna mtu wa kutufundisha na kwa ufupi, tunaongoza barani Afrika kwa kutenga maeneo zaidi ya asilimia 32.2 ya eneo lote la Tanzania (limetengwa kwa ajili ya uhifadhi)," alisema.

Kwa mujibu wa Rais Magufuli, kukamilika kwa mradi huo kutasaidia gharama za umeme kushuka, kuwapo kwa umeme wa uhakika na wa kutosha ambao utakaa kwa zaidi ya miaka 60 na gharama za uzalishaji wake zitakuwa chini zaidi ya vyanzo vingine yakiwamo makaa ya mawe na upepo.

Alisema mradi huo pia utakuwa kichocheo cha kukuza sekta ya viwanda kutokana na kupunguza gharama za uzalishaji wa bidhaa na hivyo kuongeza idadi ya wajasiriamali watakaoanzisha viwanda.

Rais Magufuli alisema mradi huo pia utaongeza kasi ya uwekezaji katika sekta mbalimbali nchini, hivyo kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na viwanda nchini na kusaidia utunzaji wa mazingira yanayoharibiwa kutokana na mahitaji ya mkaa.

Alisema umeme wa bei nafuu utarahisisha kusaidia kuhifadhi misitu kwa kuwa matumizi ya kuni na mkaa yatapungua nchini.

Alisema sekta ya utalii pia itapata manufaa makubwa kwa kuwa wanyamapori watakuwa wanapata maji katika bwawa hilo.

**RIPOTI YA CAG**

Ripoti ya CAG kuhusu Ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha 2015/16, ilibainisha kukosekana kwa mfumo madhubuti wa kudhibiti malipo ya huduma za hoteli za kitalii nchini.

Katika ripoti yake hiyo, CAG Prof. Mussa Assad, alisema changamoto hiyo inafifisha mchango wa sekta ya utalii kwenye uchumi wa nchi. CAG Assad alikabidhi ripoti hiyo kwa Rais Magufuli, Ikulu jijini Dar es Salaam Machi 27, 2017 na baadaye kuiwasilisha bungeni, Dodoma Aprili 13.

Katika ripoti hiyo (ukurasa wa 23 na 24), Prof. Assad alibainisha kuwa serikali inapoteza mapato kwenye mikataba ya upangishaji hoteli, nyumba za kupangisha na kambi za kulala watalii kwa kukosa chombo cha kufuatilia malipo ya wageni katika hoteli hizo.

CAG alisema pia katika ripoti yake hiyo kuwa wenye hoteli, nyumba za kupangisha na kambi za kulala watalii, wanapaswa kuilipa serikali kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) tozo ya kuendesha biashara ndani ya eneo la hifadhi. Pori la Akiba la Selous haliko chini ya Tanapa.

Prof. Assad alibainisha kuwa mapato ya serikali kwenye eneo hilo yanatakiwa kukusanywa kwa kutoza asilimia 10 ya malipo ya kila mteja kwenye hoteli kwa siku au kiwango maalum kilichokubalika.

Hata hivyo, CAG Assad katika ripoti hiyo alibainisha kuwa ukaguzi wake ulibaini taarifa za wateja wanaolala ndani ya hifadhi zinahifadhiwa na kutolewa na wamiliki wa hoteli, nyumba za kupangisha na kambi zilizopo.

"Mamlaka (Tanapa) haina utaratibu wa kuhakiki usahihi wa taarifa husika wanazopata kutoka kwa wamiliki wa sehemu hizo za malazi. Hii inapelekea mamlaka kutegemea zaidi na kutumia taarifa kutoka kwa wamiliki wa hoteli hizo," Prof. Assad alibainisha.

Alisema hali hiyo inaashiria kupotea kwa mapato ya mamlaka kutokana na menejimenti ya hifadhi kutokuwa na uwezo wa kuhakiki usahihi na ukamilifu wa taarifa kutoka kwa wamiliki wa hoteli hizo.

Kutokana na changamoto hiyo, CAG Assad alishauri menejimenti ya Tanapa kuwa na chombo cha kuiwezesha kuhakiki usahihi na ukamilifu wa taarifa za wageni kama zinavyotolewa na wamiliki wa hoteli hizo.

Prof. Assad pia alishauri kuwe na kiwango maalum cha tozo hizo ili kuondokana na udanganyifu unaoweza kufanywa na wamiliki wa hoteli na mabanda ya kulaza watalii.

●**Imeandikwa na Mary Geofrey na Sanula Athanas**


## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana za wadaiwa sugu kwa tarehe kama ilivyopangwa katika jedwali na muda ni kuanzia saa nne asubuhi. Mnada huo utaendeshwa na Madalali tajwa hapo chini kwa niaba ya **TUJIJENGE TANZANIA LTD**

| JINA LA MDAIWA/ MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA | JINA LA DALALI |
|---|---|---|---|---|
| Asha Abdallah Ngoteyega | Kiwanja | Msangani -Kibaha | 09/8/2019 | TAVIR A/Mart |
| Amir Mohamed Njegeka | Nyumba | Bungu 'A' Ikwiriri | 06/8/2019 | Tavir A/Mart |
| Abdul Hamad Mtimbuko | Nyumba | Ikwiriri | 06/8/2019 | TAVIR A/Mart |
| Matiku Mgaya Masabi/ Miriam J. Mallya (Mteja) | Nyumba | Kigilagila - Kiwalani | 28/8/2019 | Champion A/Mart |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana zitauzwa kama zilivyo, Mnunuzi atalipia 25% ya bei itakayofikiwa siku ya mnada, 75% italipwa ndani ya siku 14 kutoka siku ya mnada. Akishindwa kulipa,malipo ya awali hayatarudishwa.
2. Gharama za kubadilisha Hati za Umiliki zitakuwa juu ya Mnunuzi
3. Ukaguzi wa mali zinazouzwa utaanza siku moja kabla ya mnada na gharama za kumpeleka mteja kwenye dhamana zitakuwa juu ya mteja

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na;-**
**TAVIR A/Mart: 0717 495311;**
**CHAMPION Auctioneer:**

**TUJIJENGE TANZANIA LTD**
**MOB: 0718276859/0718068335 (HQ).**
**0654200448/0756761328**

215344602


# JPM aagiza Selous kuwa hifadhi

INATOKA UK. 4

(wa Maliasili na Utalii) Dk. Khamis Kigwangalla) yupo hapa. Nataka hii 'game reserve' (pori la akiba) likatwe libadilishwe, liwe 'National Park' (hifadhi ya taifa)," Rais Magufuli aliagiza.

Alisema eneo hilo likiwa hifadhi litavutia watalii kuja nchini na hivyo kuiingizia serikali mapato tofauti na sasa ambapo watu wanakwenda kuomba vitalu na kuwinda wanyama.

Alisema nchi nyingine zenye wanyamapori na mapori ya akiba ya serikali kama Tanzania, hawayatoi kwa ajili ya uwindaji, bali wanayafanya kuwa eneo la hifadhi ili watalii waende kutembelea na kuwapatia mapato.

"Kwa hiyo waziri, hiyo ndiyo meseji, hiyo ndiyo meseji ya leo kwamba kakaeni wizarani mzigawe hizi Km za mraba 50,000, zile 'hunting blocks' (vitalu vya uwindaji) muwaachie kule chini na kwa mujibu wa sheria, huruhusiwi kumuua mnyama akiwa mita 500 karibu na maji.

"Mkazingatie hayo ikiwezekana mwongeze na mita nyingine zaidi, mlikate eneo hili mligawanye, eneo kubwa liwe national park (hifadhi ya taifa)," Rais Magufuli alisisitiza.

Alibainisha kuwa gharama za mwindaji kupewa kitalu kwa ajili ya uwindaji ni Dola za Marekani 5,000 (Sh. milioni 10) ambazo thamani yake ni sawa na nyati 10, hivyo serikali haitendewi haki kwa kukosa mapato katika eneo hilo.

# Chadema wamjibu kigogo

INATOKA UK. 2

upinzani ambao baada ya mchezo huo kutangazwa wanachangamkia kucheza 'kindimu ndimu' na wanachafuka, kama unavyojua mchezo huo hauna nyasi, ni matope, mavumbi, hawana viatu, hiyo ligi iliyotangazwa siyo saizi yetu.

"Mchezo tuliorithi kutoka kwa Baba wa Taifa ni kuweza kujitawala, kuwekeza katika huduma za afya ili watoto wetu na wake zetu wapate afya bora, tuzaliane, tuongezeke."

Ingawa Dk. Bashiru hakutaja jina la mwanachama yeyote wa CCM aliyemlenga, kauli yake ilitoka ikiwa ni siku chache baada ya makatibu wakuu wastaafu wa CCM, Abdulrahman Kinana na Yusuph Makamba, kutoa waraka wao kwa pamoja wakilalama kudhalilishwa na mtu anayejiita mwanaharakati huru.

Kiongozi huyo wa CCM alisema ligi iliyotengenezwa ndani ya chama hicho si ya saizi yao, akisisitiza kiko madhubuti na viongozi wake wako imara.

Alisema kuna taratibu za kukosoana kwa nidhamu na kuwataka wanaoendekeza malumbano hayo waache alichokiita utoto.

"Sisi uongozi mzima wa chama chetu, chama ni imara kimuundo, kimfumo, kiitikadi, kifalsafa na kiuongozi, wapuuzeni hao wapumbavu, hatuogopi kukosolewa, hatupo tayari kudharauliwa, kutukanwa na kubezwa na kuitwa majina ya kejeli kwa watu ambao hawana shukrani, hatujafunzwa wala kuzoea hivyo.

# Bashiru awasha taa

INATOKA UK. 3

visingizio, wachape kazi ya siasa na kuyatafutia ufumbuzi matatizo yanayowakabili. Hata hivyo, Bashiru alisema kuna haja Watanzania wengi kuhamasishwa kushiriki katika uchaguzi ili siku ya kupiga kura kuwe na ushiriki mkubwa wa wananchi.

"Mwaka huu uchaguzi wa serikali za mitaa tunaufanya tukiadhimisha miaka 20 ya kifo cha Baba wa Taifa, tupige kura ya kuishindisha CCM kama namna ya kumkumbuka Baba wa Taifa, ni matokeo ya nchi aliyoiasisi," alisema.

Aliwahimiza vijana kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika daftari la wapigakura na kuuagiza Umoja wa Vijana wa chama hicho (UVCCM) kufanya kazi ya kuhamasisha kujiandikisha na kupiga kura. "Kuna watu wanafikiri ni migogoro na migongano, wakati wa CCM inapotafuta dola, kaa kando, kaa chonjo, mikakati hiyo siyo ya kawaida, tujiandae vizuri," alisema.

Kiongozi huyo alibainisha kuwa tayari Kamati Kuu ya CCM imeteua kamati chini ya Makamu Mwenyekiti, Philipo Mangula, kwa ajili ya kuandaa mwelekezo wa sera za CCM 2020/30 na Ilani ya uchaguzi wa mwaka 2020/25.

"Tunakaribisha maoni kwa Watanzania wote kwasababu nyaraka hizi ni za kisera, wanaCCM na wasio wana CCM tuleteeni maoni yenu kwa changamoto zinazotukabili, hata vya upinzani leteni maana ndo ilani itakayoshinda, tunataka ushirikishaji, hata Benki ya Dunia leteni, mradi yazingatie itikadi zetu," alisema.

# Uchaguzi wa UVCCM wafutwa, kisa mlungula

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

KAMATI ya siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Hanang' mkoani Manyara, imeufuta uchaguzi wa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana (UVCCM) wa wilaya hiyo, kufuatia madai kuwa rushwa ilitawala wakati wa kampeni ya kujaza nafasi hiyo.

Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Hanang', Mathew Dareda, akizungumza juzi alisema uchaguzi huo uliokuwa ufanyike Jumamosi iliyopita umefutwa na kamati ya siasa ya wilaya hiyo.

Uchaguzi huo mdogo ulikuwa ufanyike ili kuziba nafasi ya aliyekuwa Mwenyekiti wa UVCCM wa Wilaya, Ester Mchome, ambaye ameajiriwa serikalini na Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, kuwa Ofisa Mtendaji Kata ya Bargish.

Darema alisema baada ya kuona vitendo vya rushwa vimeenea kwa baadhi ya vijana wanaogombea nafasi hiyo waliamua kufutilia mbali uchaguzi huo.

Alisema kamati ya siasa ya wilaya ya Hanang' ilikaa na kuamua kufuta uchaguzi huo baada ya kuona viashiria vya matumizi makubwa ya fedha kwa baadhi ya wagombea wa nafasi hiyo ya Mwenyekiti wa UVCCM wa Wilaya ya Hanang'.

"Kwa ngazi ya kupitisha sisi wilaya tuliwapitisha wagombea hao watano ila kamati ya siasa ya mkoa ilirudisha majina ya wagombea wote watano badala ya watatu ndiyo hali hiyo ikatokea ikabidi tufutilie mbali uchaguzi huo," alisema Darema.

Alikemea vitendo vya rushwa kwenye chama hicho na kudai kuwa huo ni ujumbe kwa wanachama wote wa CCM watakaogombea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa katika wilaya hiyo.

Wagombea wa nafasi hiyo walikuwa vijana watano ambao ni Mwinyi Bajuta, Emmanuel Gamasa, Marsuet Nicodemus, Angela Nico na Halima Said.

Kwa mujibu wa Darema uchaguzi mwingine unatarajiwa kupangiwa tarehe mwezi Agosti ili vijana wajaze nafasi hiyo ya Mwenyekiti wa UVCCM wa Wilaya ya Hanang'.

Mgombea wa nafasi hiyo, Mwinyi Bajuta wa Kata ya Ganana, alipongeza hatua ya kufutwa kwa uchaguzi huo na Emmanuel Gamasa wa kata ya Balang'dalalu alisema hana cha kuzungumza juu ya hatua hiyo.

Mgombea Marsuet Nicodemus wa Kata ya Endasak, alisema walipewa taarifa kuwa kuna kampeni chafu zimefanyika na Angela Nico wa kata ya Gendabi aliridhia kusitishwa kwa uchaguzi huo kutokana na viashiria vya rushwa vilivyoonekana.

"Walichofanya viongozi wa CCM ni jambo sahihi kwani awali kabla ya kuanza kwa mchakato wa uchaguzi huo tulipochukua fomu tuliambiwa tufuate kanuni na taratibu za uchaguzi," alisema Angela.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Yefred Myenzi, akizungumza na wadau wa elimu wa wilaya hiyo, juzi, akiwataka kuwa wazalendo. **PICHA: GIFT THADEY**

# Ugunduzi chuo kikuu uanzishe viwanda

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mtakatifu Joseph, wameshauriwa kutumia teknolojia ya ugunduzi wanayofundishwa vyuoni kuanzisha viwanda vidogo ili kufanikisha azma ya taifa kuingia kwenye uchumi wa kati.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, mara baada ya kukagua kazi za ufundi za aina mbalimbali, zilizofanywa na wanafunzi wa chuo hicho.

Kazi hizo ziko kwenye maonyesho ya teknolojia yaliyoandaliwa na Chuo cha Mtakatifu Joseph, kinachotoa elimu ngazi ya cheti na shahada kwenye fani ya uhandisi, afya, sayansi ya kompyuta na ualimu wa sayansi.

Alisema wanafunzi hao wameonyesha kuiva katika ubunifu wa vitu mbalimbali ambavyo vinawezesha kuanzisha viwanda.

"Kama hapa nimeona mashine za kukata vyumba, kukata na kutoa utumbo wa samaki na teknolojia ya kumfuatilia mtu anapokuwa anafanya mambo mbalimbali au kazi tofauti na hii ni muhimu ofisini.

Ni tofauti na ile ya kuweka vidole ambayo unaweza kuweka ukaonekana umeingia ukaja muda wa kutoka ukabonyeza tena lakini teknolojia hii haiwezi kudanganya unaonekana kila unapokuwa,"alisema Kitwega.

Aliwaambia kuwa teknolojia hizo zinatoa majibu kwa jamii na kutatua tatizo la ajira kwa wanafunzi, kwani mwanafunzi akimaliza hapo anajiajiri mwenyewe.

Aidha, alitoa wito kwa vyuo binafsi kushirikiana na serikali kuongeza kiwango cha udahili wanafunzi na hasa wa sayansi, ila kwa kuzingatia utoaji elimu bora inayokidhi viwango vya soko la sasa.

"Lakini vyuo hivi lazima viboreshwe miundombinu yake ili tupate wanafunzi wengi wanasayansi watakaojiunga huko na hatimaye taifa lifikie lengo lake la kuwa na nchi ya viwanda na kufikia uchumi wa kati,"alisema.

Alitumia fursa hiyo kupongeza chuo hicho kwa kazi kubwa ya kuwatengeneza vijana kuwa wabunifu katika nyanja mbalimbali kwa kutengeneza mashine za aina mbalimbali zenye kuhitajika katika jamii.

Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo cha Mtakatifu Joesph, Prof. Innocent Ngalinda, alisema wamekuwa wakifanya kila mwaka maonyesho hayo Dar es Salaam, lakini kwa mwaka huu wameamua kuzunguka mikoani, lengo likiwa kuhakikisha wanawafikia wanafunzi wengi zaidi na kuwahamasisha kupenda masomo ya sayansi.

"Tunaamini wanapoona maonyesho yetu na kazi za ubunifu za wenzao walizofanya, watahamasika na kubadili mtazamo wa kuchukia masomo ya sayansi na kuyapenda na hatimaye kujiunga katika chuo hiki na vingine vya sayansi,"alisema Profesa Ngalinda.

Alisema chuo chao kinajikita kumwandaa mwanafunzi kujiajiri baada ya masomo na kuachana na dhana ya kutegemea kuajiriwa pekee.

Akitoa mfano alisema kuna wahitimu wao ambao wapo tayari kuanzisha viwanda vidogo kwani wapo wanaotengeneza uzalishaji wa umeme wa jua, upepo, mashine za kukata na kutoa utumbo samaki, kuchenjua madini na mashine za kukata vyuma.

"Sasa hivi tunaona vijana wetu wengi wamekosa hamasa ya kuchukua masomo ya Sayansi, lakini tunaamini wakiona kwa vitendo kazi za wanasayansi watahamasika kupenda masomo hayo,"alisema Profesa.

Mmoja wa wanafunzi wa kike aliyoonyesha kazi za ubunifu wake ni Faraja Bwashe, ambaye alivuta watu kwa kuonyesha mashine ya kukata vyuma na mabati ambayo wengi walivutiwa na kuomba kutengenezewa.

# Hudumieni wazee bure, haraka - DC

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Murro, ameagiza kuwa kuanzia sasa wazee wote watakaokwenda katika vituo vya afya, wapewe huduma bure na kwa haraka.

Aidha, hata kama mzee atakuwa amesahau kitambulisho kinachomtambulisha, au bima ya afya apatiwe huduma kwanza, ndiyo mengine yafuate.

Aliyasema hayo jana wakati wakiongea katika mkutano ulioandaliwa na Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, ulioshirikisha wazee wa kimila, viongozi wa dini, pamoja na viongozi wa vyama mbalimbali vya siasa.

Wazee hao walimwomba kuwasaidia kupatia vitambulisho vya wazee, vitakavyo wawezesha kupatiwa huduma za afya bure popote pale wanapopata matatizo ya kiafya.

Aidha, waliiomba serikali kuwasaidia kupata msaada wa kunusuru kaya maskini na zisizojiweza unaotolewa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf ).

Walieleza kuwa katika vijiji vyao hawajapatiwa msaada huo na kuna wanavijiji wengi ambao ni maskini na wasiojiweza.

Walisema kwa muda mrefu wamekuwa wakikumbana na changamoto mbalimbali zikiwamo za ubovu wa miundombinu ya barabara gharama kubwa ya maisha na ukosefu wa mitaji.

Aidha, waliomba Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kuwasogezea huduma ya kupata vitambulisho hivyo karibu, kwani sehemu ambayo wameipanga watu waifuate ni mbali na inawapa changamoto kubwa wazee hao kufika.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, aliwashukuru wazee hao, kwa kupokea wito wake huku akitaja kuwa lengo ni kusikia changamoto mbalimbali zinazowakabili wazee na kupanga jinsi ya kuzitatua na kupata ushauri kutoka kwao kwani wazee ni hazina.

Aliwahakikishia wazee hao kutatua kero zao zote, ambazo wamezitaja kuanzia kero za vitambulisho vya huduma za matibabu kwa wazee na aliagiza kuanzia sasa wazee wote watakaokwenda katika vituo vya afya, wapewe huduma bure na kwa haraka.





# Wataka kodi kamba kutoka nje

**Na Godfrey Mushi,** SAME

WAZALISHAJI wa mkonge nchini, wameiomba serikali kuangalia uwezekano wa kutoza kodi kubwa zaidi kwenye kamba bandia zinazoingizwa nchini kwa wingi kiasi cha kuhatarisha soko la ndani.

Hayo yamo katika taarifa iliyopelekwa Ofisi ya Waziri Mkuu na Mshauri na Meneja wa kiwanda cha kuchakata mkonge cha Hassan Sisal Estates kilichopo kwenye mashamba yanayomilikiwa na Kampuni ya Mohamed Enterprises (MeTL) Same, mkoani Kilimanjaro.

Taarifa hiyo iliyoandikwa na mshauri na meneja wa kiwanda hicho, Ndekirwa Nyari, imeeleza kuwa wakiwa wadau wa uzalishaji wa zao hilo, wanaiomba serikali kuongeza kodi katika kamba bandia, au kupiga marufuku kama ilivyofanya kwa mifuko ya plastiki.

"Tatizo kubwa tulilo nalo ni hii changamoto ya kamba bandia ambazo zinakuja kwa wingi sana sasa hivi. Kwanza niipongeze serikali kwa hatua yake iliyochukua kuzuia mifuko ya plastiki.

"Na hizi kamba bandia, ingekuwa vizuri serikali ikaangalia aidha kutoza kodi kubwa kwenye hizo kamba zinazoingia nchini au kupiga marufuku kama ilivyopiga kwa mifuko ya plastiki na tunafikiri kwamba ajira zitaongezeka pamoja na matumizi ya mifuko tunayozalisha itaongezeka sana," imeeleza sehemu ya taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa mshauri huyo wa mkonge, mashamba makubwa ya katani yanauza nje ya nchi asilimia 80 ya zao hilo kama mkonge ghafi na asilimia 20 pekee ndiyo inayokwenda kwenye viwanda vya ndani.

Alisema kiwanda hicho kinachakata mkonge kwa ajili ya kutengenezea kamba za kufungashia pamoja na kamba za kutengenezea magunia.

"Kama Kiwanda cha Amboni, hiki kinasokota tani 6,000 kwa mwaka. Kiwanda chetu cha kusokotea mkonge kilichoko Dar es Salaam kina uwezo wa kutumia tani 3,000 na Ngomeni Tanga kina uwezo wa kuchakata tani 6,000. Matumizi ya mifuko tunayozalisha itaongezeka sana. Hata hivyo shamba hili limeajiri wafanyakazi 500," iliongeza taarifa hiyo.

Hivi karibuni pia, wakulima na wazalishaji wa nyuzi za mkonge mkoani Morogoro, nao waliiomba serikali kufufua kituo cha kufundishia wataalamu wa zao hilo kilichoko Mlingano, Tanga kwa kuwa hivi sasa hakuna wataalamu wa kutosha.

Wataalamu wanaohitajika katika sekta ya mkonge ni pamoja na wataalamu wa mashambani, wataalamu wa kuendesha mashine za kutengeneza nyuzi (korona) na wale wa kutengeneza vipuri vya mashine hizo.

Pamoja na mambo mengine, wadau hao wameiomba pia serikali kuongeza matumizi ya magunia katika kuhifadhi nafaka mbalimbali ili zao la mkonge liweze kupata soko.



Wafanyausafi wa Manispaa ya Kinondoni, wakifagia kuondoa mchanga katika Barabara ya Morogoro eneo la Magomeni Usalama, ijini Dar es Salaam jana. . **PICHA: JOHN BADI**

## DC apeleka kilio kwa Waziri Mkuu

**Na Godfrey Mushi, SAME**

MKUU wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, amempelekea Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, mambo matatu yanayohitaji msukumo wa ofisi yake kupata majibu ya ufumbuzi wa changamoto zilizopo, likiwamo suala la uchakavu wa miundombinu na majengo ya Hospitali ya Wilaya hiyo.

Hospitali hiyo, haijawahi kufanyiwa matengenezo tangu majengo yake yalipojengwa na wakoloni mwaka 1957.

"Tumeshampa taarifa rasmi Waziri Mkuu kwamba moja ya mahitaji yetu makubwa kwa sasa ni kutaka kuingizwa kwenye mpango mkakati wa serikali wa kujengewa hospitali mpya ya kisasa ya wilaya. Wodi ziko katika hali tete kutokana na uchakavu wa miundo mbinu," alisema.

Kwa sasa, Wilaya ya Same imeanza mkakati wa kuboresha hospitali yake ya wilaya ambayo majengo yake ni chakavu, hivyo kushindwa kuhimili ongezeko la wagonjwa wa ndani na nje ya wilaya.

Alisema licha ya uchakavu wa majengo, hospitali hiyo pia inakabiliwa na uhaba wa wodi hususani ya huduma ya uzazi.

Hospitali hiyo imekuwa ikipokea idadi kubwa ya wagonjwa kutokana na kuhudumia pia wagonjwa kutoka wilaya za jirani ambazo ni Simanjiro ya mkoani Manyara, Korogwe (Tanga) na Mwanga ya Mkoa wa Kilimanjaro.

Kuhusu uhaba wa dawa na vifaa tiba, mkuu huyo wa wilaya alisema tayari serikali imeshaongeza fedha za dawa na tiba na hivyo kupunguza malalamiko ya wagonjwa kukosa dawa.

Changamoto zingine ambazo Mkuu wa Wilaya ameomba serikali kuu kuzipatia ufumbuzi ni ukosefu wa gari la kubeba wafungwa katika Gereza la Wilaya ya Same na ofisi ya mkuu wa idara hiyo kupatiwa gari.

# Manufaa yanukia wakulima wa migomba

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) inayojihusisha na usambazaji wa teknolojia, mbinu na utaalamu wa kilimo cha kisasa kwa wakulima na wadau mbalimbali, leo inazindua rasmi mradi mpya wa uhaulishaji wa migomba katika Wilaya ya Rombo.

Mradi huo utazinduliwa na Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Agness Hokororo, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wakulima wa Migomba, inayofanyika katika Kata ya Mengeni.

Kwa mujibu wa Ofisa Uhusiano wa Tari, Ruth Mnzava, maadhimisho hayo yatatanguliwa na utoaji elimu kuhusu mradi wa uboreshaji wa migomba, maoni ya wadau wa uhaulishaji wa teknolojia, mada kuhusu umuhimu wa machapisho katika uhaulishaji wa teknolojia na ushuhuda kutoka kwa wakulima juu ya ujio wa mradi wa migomba.

"Katika kufikia uchumi wa kati unaotegemea viwanda, uboreshaji wa kilimo chetu ni suala muhimu na hii ni kwa sababu mbali na kutegemewa kuwalisha Watanzania wanaoongezeka kwa idadi mwaka hadi mwaka, kilimo cha migomba kinategemewa pia katika kutoa sehemu kubwa ya malighafi kwa ajili ya viwanda hivyo," alisema.

Tari ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge, Namba 10 ya Mwaka 2016, ikipewa jukumu la kutafiti, kusimamia na kuhamasisha matumizi ya teknolojia mbalimbali kwa wakulima na wadau wengine.

Taasisi hiyo pia imepewa jukumu kwa mujibu wa sheria za kuratibu shughuli zote za utafiti wa kilimo Tanzania Bara.

Idara ya usambazaji wa teknolojia na uhusiano ina jukumu la kuhakikisha teknolojia zote, ubunifu na mbinu bora za kilimo katika mazao yote ya kimkakati zinasambazwa ili kuwafikia wakulima na wadau wengine walioko katika mnyororo wa thamani.

Hata hivyo, idara hiyo inahusika katika kuimarisha ushirikiano na wadau wa kilimo wa ndani, kikanda pamoja na wa kimataifa katika mnyororo wa thamani.

Inaelezwa kuwa, kwa sasa kuna vituo 18 vya utafiti nchini na kila kituo, kina jukumu la kitaifa la kufanya utafiti na maendeleo ya zao moja au zaidi ya moja.



# Utekelezaji wa sheria Ukimwi wasuasua

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UTEKELEZAJI wa Sheria ya Ukimwi ya mwaka 2008 kuhusu adhabu kwa wanaobainika kuwanyanyapaa wagonjwa wa Ukimwi, umeelezwa kusuasua kutokana na waathirika wa vitendo hivyo kushindwa kujitokeza kwenye vyombo vya sheria kudai haki zao.

Miongoni mwa adhabu zinazotolewa na sheria hiyo kwa wanaofanya vitendo vya unyanyapaa ni kifungo cha miezi mitatu hadi sita jela au faini ya Sh. 500,000 ama vyote kwa pamoja.

Ofisa Sheria Mwandamizi wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (Tacaids), Miraji Mambo, alisema hayo jana katika kikao cha wadau wa afya, Mahakama, Polisi na wawakilishi wa Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (Nacopha) ambacho kinalenga kuwaelimisha kuhusu sheria za Ukimwi na haki za binadamu.

Alisema pamoja na kuwapo na adhabu, iwapo mtumishi wa kada ya afya atabainika kumnyanyapaa mtu kutokana na hali yake ya kiafya kumekuwa na changamoto kwa wanaotendewa kutokufika mahakamani kwenda kutoa ushahidi.

"Katika utoaji wa huduma za Ukimwi kumekuwa na ubaguzi na unyanyapaa ambao unafanywa na watumishi wa kada ya afya licha ya Katiba, Sheria ya Ukimwi na miongozo mbalimbali kutolewa," alisema.

Mambo alisema inapothibitika mtu amenyanyapaliwa kutokana na hali yake, Sheria ya Ukimwi kuna adhabu ya kutozwa faini ya kiasi hicho cha fedha pamoja na kifungo.

"Changamoto kutokana na hali ya unyanyapaa inayofanyika katika jamii watu wanaofanyiwa vitendo hivyo hawajitokezi mara kwa mara na wanapojitokeza kesi haisikilizwi hadi mwisho kutokana na anayetendewa anaogopa kutoa ushahidi, hali inayofanya Hakimu kufuta kesi kutokana na kutofika mahakamani," alisema.

Aliwataka watumishi wa kada ya afya kutoa huduma kwa wagonjwa hao bila ubaguzi na kujiepusha na unyanyapaa.

Naye Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Wilaya ya Kongwa, Saguda Kisasila, alisema mashauri mengi ya unyanyapaa kwa wagonjwa hao hayafiki mahakamani kutokana na watendewa kutojitokeza polisi kushtaki.

"Ni mara chache sana kukutana na adhabu za aina hii kutokana na watendewa kutofika polisi na mahakamani na wakati mwingine ni kutokana na watendewa kutojua sheria," alisema.

Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto kutoka Manispaa ya Mpanda, Muna Sumry, alikiri kuwa wakati mwingine wahudumu na wagonjwa wamekuwa wakitofautiana kwenye mazungumzo kuhusu utekelezaji wa haki za mtoa huduma na mgonjwa.

Kadhalika, Katibu wa Nacopha Konga ya Temeke, Japhes Kaiteni, alisema sheria hiyo ina upungufu katika utekelezaji ikiwamo kukosa kanuni za kuisimamia.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, SACP Gilles Muroto, akijaribu kuendesha moja ya pikipiki mbili alizopokea msaada kutoka kiwanda cha kutengeneza pikipiki cha Wuzhou Investment Ltd, cha Mkuranga, mkoani Pwani, katika hafla iliyofanyika ofisini kwake, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mavunde aagiza alama barabarani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, amezitaka mamlaka zinazohusika na miundombinu ya barabara, kuweka alama ili kuwasaidia watumiaji kuondokana na ajali ambazo zimekuwa zikiongezeka kila kukicha.

Mavunde aliyasema hayo jana alipokuwa akitoa zawadi kwa washindi wa michoro ya usalama barabarani ikiwa ni sehemu ya kuhitimisha mafunzo ya usalama barabarani yaliyoandaliwa na kamapuni ya Puma Energy Tanzania kwa wanafunzi 4,500 wa shule tano za jijini hapa.

Alisema kuwapo kwa alama za barabarani kutasaidia kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikijitokeza katika maeneo mbalimbali hasa kwa wanafunzi ambao wamekuwa wakigongwa na kupoteza maisha na madereva bodaboda.

Kwa mujibu wa Mavunde, wanafunzi ambao wamekuwa wakivuka barabara kila siku wakati wa kwenda shule au kurudi nyumbani wamekuwa hatarini kupoteza maisha yao kutokana na ajali za barabarani.

"Kwa mfano hapa Dodoma barabara nyingi sana zimejengwa kwa kiwango cha lami, lakini bado lipo tatizo la ukosefu wa alama barabarani na nyingi zimepita katika makazi na taasisi kama shule, hivyo ni lazima zile ambazo ziko chini ya Tarura (Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini) waweke alama na zile ambazo ziko chini ya Tanroads (Wakala wa Taifa wa Barabara) ziwekewe alama ili kupunguza ajali nchini," alisema.

Aidha, Mavunde aliahidi kuweka alama katika barabara ambazo zimepita katika maeneo ya shule ili kuwawezesha wanafunzi kuvuka katika mazingira salama wakati wanakwenda shule au kurudi nyumbani.

"Nimeongea na Meneja wa Tarura anipe gharama za kuweka alama katika barabara hizi ambazo zimepita katika shule hizi za msingi ili mimi kama mbunge nilipie gharama za kupaka rangi katika barabara hizo zilizopita katika shule," alisema.

Mavunde aliitaka Kampuni ya Puma Energy Tanzania kupanua wigo wa mafunzo ya usalama barabarani katika shule nyingi nchini.

"Lakini pia nitoe wito kwenu mwanzishe programu ya kufundisha walimu wa shule zetu za msingi ili waweze kuwafundisha vijana wetu katika shule zao wakati wanapofundisha masomo mengine," alisema Mavunde.

Naye Mratibu wa Mafunzo hayo kutoka shirika lisilo la kiserikali la Amend, Neema Swai, alisema lengo lao ni kuwajengea uelewa wanafunzi katika shule za msingi ili kuondokana na ajali.

Alisema jamii imekuwa na mtizamo kuwa ajali haina kinga wakati ukweli ni kwamba ajali nyingi zinazotokea upo uwezekano mkubwa wa kuzizuia.

Swai alizitaja shule zilizoshiriki katika mafunzo hayo kuwa ni Kizota, Kaloleni, Mnadani, Mazengo pamoja na Jenerali Msunguli zote za jijini Dodoma.

# Waomba utatuzi mgogoro wa ardhi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKAZI wa Kitongoji cha Azimio, Kata ya Ipala jijini Dodoma, wameiomba Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuingilia kati mgogoro wa ardhi unaoendelea baina yao na uongozi wa kijiji na kata.

Wakizungumza jana kwa nyakati tofauti, wananchi hao walisema uongozi huo umekuwa ukiwazuia kuendeleza, kuuza ardhi yao ya asili huku wakidai kuwa eneo hilo lina matumizi ya serikali.

Mmoja wa wakazi hao, John Nzuga, alisema wakati wa iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA) ilitaka kutenga eneo hilo hadi Hombolo kwa ajili ya matumizi ya serikali, lakini wananchi walikataa.

Alisema eneo hilo kila wakati limekuwa likipangiwa matumizi na baada ya Rais Magufuli kutangaza Dodoma kuwa makao makuu ya nchi, uhitaji wa ardhi umeongezeka nao wanahitaji kuuza vipande vya maeneo yao ili kujikimu na kuboresha makazi yao.

"Lakini viongozi ambao tumewachagua wenyewe kwa kuwapigia kura wanatufanyia mizengwe wanatuzuia," alisema.

Naye Andrea Makocho alisema tangu azaliwe hakuwahi kuishi nje ya Ipala na hawakuwahi kukubaliana na uwepo wa hifadhi kwenye makazi yao hayo.

"Nimezaliwa hapa, siku hizi hawa viongozi wananishangaza sana, wanasema hata ukiwa na shida usiuze kwa sababu eti ni eneo la serikali," alisema. Nao baadhi ya wananchi walionunua maeneo kwenye eneo hilo, kabla hawajanunua walikwenda na wataalamu wa ardhi kutoka ndani ya ofisi za Jiji, ili kujiridhisha juu ya usalama wa maeneo husika.

"Mimi nilimlipa ofisa Sh. 50,000 nikaja naye akiwa na GPS akachukua vipimo na kurudi ofisini kwake kusoma ramani, kisha akanihakikishia kuwa eneo hilo ni salama kwani ramani ya mipango miji haijafika, hivyo nikinunua itakapofika itanikuta nikiwa miongoni mwa wakazi wa eneo hilo," alisema Saida Mohamed.

Alisema baada ya kupata uhakika, alinunua eneo lenye ukubwa wa ekari nne huku mwenyekiti wa kitongoji akiwa shahidi.

Akizungumzia malalamiko hayo, Mwenyekiti wa Kitongoji hicho, Gideon Mulundi, alisema awali walikubaliana na Diwani George Magawa, kufanya mkutano wa kitongoji Julai 8, mwaka huu, lakini kabla ya siku hiyo aliandikiwa barua na Mtendaji wa Kata, Herman Malindika, akitakiwa kuwaeleza wananchi kuwa mkutano huo hautakuwapo.

Alisema barua hiyo ya Julai 5, mwaka huu, ambayo Nipashe ina nakala yake, inaonyesha ombi la mkutano wa wakazi wa kitongoji hicho kutaka kufahamishwa juu ya hifadhi ndani ya makazi yao limepelekwa kwa Mkurugenzi wa Jiji, Godwin Kunambi, hivyo mkutano huo hautafanyika.



# Waziri aonya dharau kwa walimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewataka maofisa na walimu kuacha tabia ya kudharau walimu wanaofundisha masomo ya sanaa kwa kuwa yote yana umuhimu na ubora katika maendeleo ya nchi.

Akizungumza juzi na walimu wa shule za sekondari za wilaya ya Micheweni, Pemba, alisema si kila mtu anaweza kuingia maabara kufanya kazi hizo, lakini kuna sehemu nyingine watahitajika wataalamu wa lugha ili kurekebisha maneno na kufahamika.

Juma aliwataka maafisa hao kuacha tabia hiyo kwa kuwa masomo ya sanaa na ya sayansi yote yako ndani ya mitaala ya elimu na yanakubalika kisheria na ni wajibu wa wote kusimamia kwa pamoja. Alisema tatizo lililopo ni kuwa wataalamu na walimu wa masomo ya sanaa wako wengi kulinganisha na wasayansi ndiyo maana serikali imekuwa ikitilia mkazo wanafunzi kusoma masomo ya sayansi ili kupunguza tatizo la kuagiza walimu wa masomo ya sayansi nje ya nchi.

Alisema Rais wa Zanzibar anapotoa nafasi za serikali za masomo nje ya nchi, kawaida anazitoa sawa kwa masomo ya sanaa na sayansi, lakini zinapokuja za nje ya nchi zinatokana na nchi yenyewe inafundisha kwa mujibu wa fani walizo nazo. Pia aliwataka maofisa hao kushirikiana na walimu, wazazi na wanafunzi katika kuhakikisha mafanikio ya watoto yanapatikana na kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi.

Waziri pia aliwataka walimu kufanya kazi kwa kuzingatia maadili na kuacha kuchanganya kazi na siasa kwani wanaweza kuwapotosha wanafunzi.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Idrissa Muslim Hija, alisema haiwezekani kila mwanafunzi anayefeli kupelekwa katika vyuo vya ufundi kwa kuwa kuna mashine na vifaa mbalimbali vinatumiwa, hivyo wanafunzi wanaojiunga na vyuo hivyo wanatakiwa wawe wenye uwezo wa kutambua.

Alisema wizara hivi sasa imeandaa utaratibu maalum kwa wanafunzi ambao watamaliza kidato cha pili watapelekwa katika vyuo hivyo vya mafunzo ya ufundi ili kuweza kupata ujunzi.

Kwa upande wake, Ofisa Mdhamini wa Wizara ya Elimu Pemba, Mohammed Nassor, alisema kuwapo uchache wa mabweni kisiwani Pemba kwa wanafunzi kunatokana na ongezeko la wanafunzi hali ambayo imesababisha bweli lililopo kutokidhi mahitaji.

Kwa upande wao, walimu na maofisa hao wameishauri Wizara ya Elimu kuangalia uwezekano wa kufanya makongamano na kujadili maendeleo ya elimu nchini ili kujua changamoto za sekta hiyo hali ambayo inasababbisha kila mwaka Zanzibar kuwa na shule za mwisho zinazofanya vibaya katika mitihani ya taifa.

Walimu hao walisema kuwapo kwa maendeleo ya sayansi na teknolojia imekuwa tatizo kwa wanafunzi na huwaathiri katika kutumia teknolojia hizo kwa mambo yasiyowahusu badala ya kutumia kwa masomo.



Wakazi wa jiji, wakichagua sidiria za mtumba zinazouzwa kando ya Barabara ya Morogoro, eneo la Manzese, jijini Dar es Salaam jana, licha ya serikali kupiga marufuku matumizi ya nguo hizo. **PICHA: JOHN BADI** .

# Makamu wa Rais ataka tahadhari majanga

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANANCHI wametakiwa kuchukua tahadhari ya kujiepusha na majanga yanayoweza kuepukwa ili kuendelea kubaki salama katika maisha yao.

Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza wakati akiwafariji na kuwapa pole wananchi wa kijiji cha Shumba Mjini kisiwani Pemba baada ya kupata msiba wa kufariki dunia jamaa zao wawili kutokana na upepo mkali uliovuma wakiwa katika shughuli za uvuvi.

Alisema hakuna chombo chochote kinachoweza kupambana na mchafuko ya hali ya hewa yanapojitokeza maafa, lakini jamii inatakiwa ichukuwe tahadhari mapema ili kupunguza madhara.

Balozi Iddi aliitaka jamii kuwa na utaratibu wa kufuatia taarifa zinazotolewa na mamlaka ya hali ya hewa nchini ili kuweza kuepukana na maafa ambayo yanaweza kuepukika.

Aliwataka wananchi waliokumbwa na majanga hayo kuwa na moyo wa subira katika kipindi hiki cha msiba wa jamaa zao.

Naye Mwakilishi wa Micheweni, Shamata Shaame Khamis, alisema vyombo vya dola kisiwani Pemba kwa kushirikiana na wananchi, vilifanya jitihada za kuwatafuta wavuvi waliopotea juzi baada ya vyombo vyao vya uvuvi kukumbwa na dhoruba kali.

Alisema wavuvi wanne waliokuwamo kwenye boti wameokotwa Mombasa nchini Kenya na mmoja kati yao alikuwa tayari ameshafariki dunia.

Katika hatua nyingine, Balozi Iddi alipata fursa ya kukikagua kisima cha majisafi na salama kilichochimbwa na Taasisi ya Pemba Foundation na Mamlaka ya Maji Zanzibar (Zawa) kwa ajili ya wananchi wa visiwa vya Fundo na Uvinje, Pemba.

Kisima hicho kilichochimbwa katika kijiji cha Ukunjwi kitasambaza maji katika visiwa hivyo baada ya mfumo wa mwanzo uliowekwa na Zawa kusita kutokana na kuharibika kwa tangi kubwa la kuhifadhia maji.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Pemba, Omar Mshindo Bakari, alisema kisima hicho chenye uwezo wa kutoa maji lita 40,000 kwa saa kitaanza huduma yake ifikapo Novemba, mwaka huu na kuondosha tatizo la ukosefu wa huduma ya maji katika visiwa hivyo. Balozi Iddi alisema nia ya serikali ni kuona inafanikiwa katika kuwahudumia wananchi wake hasa katika upatikanaji wa maji safi na salama mahali popote.

# Wanawake kuwezeshwa katika umiliki wa ardhi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MRATIBU wa Mradi wa Kuwawezesha Wanawake katika Umiliki wa Ardhi kutoka Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (Tamwa) Zanzibar, Winifrida Atua, amesema watawajengea uwezo wanawake ili kudumu gharama za ufuatiliaji wa umiliki ardhi kisheria.

Akizungumza katika mafunzo ya wajasiriamali wa kutengeneza sabuni na majani ya chai jana, alisema Tamwa imewapa mafunzo wajasiriamali 15 ili wao wawe walimu kwa wajasiriamali walioko katika maeneo yao ambao watafanya biashara hiyo na kuwaingizia kipato.

Atua alisema wajasiriamali hao wanafundishwa namna ya kutengeneza bidhaa zenye ubora na kiwango ili kuendana na masoko yaliyopo na kujikomboa na umaskini kupitia bidhaa hizo.

Mratibu huyo alisema katika mradi huo wa kuwawezesha wanawake kumiliki ardhi kisheria wameona changamoto kubwa zinazowakumba wanawake hao kushindwa kumiliki ardhi ni kutokana na kutomudu gharama za ufuatiliaji wa umiliki ikiwamo fomu na mambo mengine.

Nao wajasiriamali wanaopatiwa elimu hiyo, walisema kupitia mafunzo hayo, wamejua namna ya kutengeneza sabuni zenye ubora na kiwango ili kuwavutia wateja.


Nachoum Othman, mmoja wa wajasiriamali hao, alisema awali walikuwa hawajui vipimo sahihi vinavyotakiwa katika utengenezaji wa sabuni hali iliyosababisha sabuni zao kutokuwa na kiwango kama kinachohitajika na Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS).

Naye mjasiriamali Saum Ali alisema kutokuwa na vitendea kazi sahihi ni changamoto inyowakumba wajasiriamali wa sabuni na kushindwa hata kutengeneza sabuni zinazohitajika.

Mkufunzi wa mafunzo hayo, Mohammed Musaa, alisema changamoto iliyopo kwa wajasiriamali wengi wa Zanzibar hususan wa sabuni na majani ya chai ni kutojua vipimo halisi vya kutengeneza sabuni na vifungashio kutokuwa na ubora.

Alisema hali hiyo imesababisha wajasiriamali hao kuzalisha sabuni zisizo za viwango vinavyokubalika na ZBS pamoja na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI
TELE



**MENEJA: 'SITOMWACHA R KELLY PEKE YAKE'** Soma UK.15

JUMAMOSI JULAI 27, 2019



# UTATA 'THE LION KING' Lupita kawa chambo

## BASI SAWA



# Magreth kuzindua 'Salamu kwa Yesu'

MWIMBAJI nyimbo za Injili, Magreth Sagini, amesema kuwa anapenda kutumia nyimbo zake kupunguza maovu na kuchochea neema za Mungu.

"Katika ujio wa albamu nimeimba ili kuchochea watu kukumbuka zaidi wema wa Mungu kwani jamii imekuwa bize sana na harakati za mambo ya kidunia,"alisema Magreth.

Magreth meongeza kuwa Julai 4 mwaka huu atazidua albamu yake 'Salama kwa Yesu' yenye jumla ya nyimbo nane katika ukumbi wa DMC Tabata Segerea huku akisindikizwa na waimbaji kama Elizabeth Nshimanje ,Afred Funda ,Mariam Kilenyi.



# Lil Ommy kuwania tuzo Star QT Award

MTANGAZAJI wa kipindi cha burudani wa radio cha Times FM, Omary Tambwe, maarufu kama Lil Ommy, ametajwa kuwania tuzo kubwa za Star QT Awards 2019.

Lil Ommy ameingia katika kipengele cha Mtangazaji bora barani Afrika mwaka 2019, Kupitia kipindi chake cha The Playlist.

Akizungumzia tuzo hizo, Lil Ommy 'The MVP', amesema Star QT Awards zinatolewa kwa mwaka wa sita sasa na amefurahi kuwa miongoni mwa mastaa kutoka Tanzania wanaowania tuzo hizo.



# Shilole hatanii kusafiri kwa baiskeli

WIKI hii mwanamuziki na mwigizaji, Shilole, ametawala katika mitandao ya kijamii baada ya kuonekana akiendesha baiskeli na kutaja kuwa ni usafiri wake mpya.

Hata hivyo, msanii hiyo amezidi kuwaweka njia panda mashabiki wake kwa kusema ana ujuzi wa kuendesha chombo hicho siku nyingi.

"Usafiri wa baiskeli sikuanza sasa hivi, nilitumiaga sana huko nyuma lakini kutokana na kununua gari niliacha. Watu wasione naigiza ndio usafiri wangu kwa sasa," amesema Shilole.

## INSTA-TWITTER





**Ukifurahia** kushangiliwa ukizomewa pia furaia na usipanick angalia mbele na muombe mwenyezi mungu akusaidie utashinda tu - **Ally Choki.**



**Ikiwa** kila zuri unalohitaji linakupa dhamana ya kulipigania. Basi usiwe mtu wa kuamini kwenye bahati **-Rich Mavoko.**



## UTATA 'THE LION KING'

# Lupita kawa chambo

LICHA ya kelele zinazopigwa na watu kutokea Afrika ya Mashariki kuhusu Album mpya aliyoiachia Beyonce 'The Lion King: The Gift" kuwashirikisha wasanii wa Afrika Magharibi, msanii huyo amepooza hali kwa kuisifia ngozi wa mwigizaji wa Kenya Lupita Nyong'o.

Katika kibao cha 'Brown Skin Girl' inayopatikana kwenye Album hiyo aliyomshirikisha Wizkid pamoja na mwanae Blue Ivy, Beyonce amemtaja muigizaji Lupita na kumdondoshea sifa kibao ikiwemo kusifia uzuri wake pamoja na rangi ya ngozi yake kuwa nyeusi.

Bila kukawia Lupita alitoa shukrani zake za dhati na kusema "Asante Beyonce kwa hii zawadi"




**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

**@burudanitele**

## UNASEMAAA...

# Mwasiti 'Perfomance' yake tamu

MKONGWE wa muziki wa Bongofleva, Mwasiti, amewababamba mashabiki wa muziki baada ya kibao chake 'Perfomance' kufanya vizuri siku chache tangu kiachiliwe hewani.

Katika wimbo huo ambao amemshirikisha rapa Gnako kutoka lebo ya Weusi, umeonekana kuwagusa wengi kutokana na mashairi na sauti za wasanii hao zilivyokuwa tamu.

"Ujio mpya wa Mwasiti hakukosea ni wimbo mzuri ambao huwezi kukaa chini kama ukipigwa," alisema Rashid Juma kupitia mtandao wa You Tube.



## BODA 2 BODA

# Mzee wa Bwax ajivunia kipaji chake



MKALI wa muziki wa Singeli, Mzee wa Bwax, amesema kipaji alichonacho kimemfanya kutobabaika kutoa singo kali kila wakati.

Akizungumza na BT, Mzee wa Bwax amesema kinachowaponza wasanii wengi wa muziki huo kupotea haraka mara wanapopata umaarufu ni kutokana na kutokuwa na vipaji badala yake wanavamia fani.

"Siri ya kudumu kileleni kwa muda mrefu ni kutumia vizuri kipaji change, kila ninapoamua kutoa singo inakuwa kali zadi tofauti na wezangu ambao wanavamia kazi kwa kuganga njaa," amesema mzee wa Bwax.

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Usiruhusu** mawazo ya watu yabadili dunia yako . Kila siku unanafasi kubwa ya kutengeneza ndoto yako. Usikubali kukatishwa tamaa na vile watu wanasema-**Muna Love.**



**Kwenye** Dunia ukifanikiwa kupiga hatua nakukataza yafuatayo. 1. Usiwe mjuji wa kila kitu. 2. Usijifanye hujui kila kitu. Ukizingatia haya nitakueleza kitakachofuata-**Madebe Lidai.**



**Kila** hali katika maisha ya mtu imetokana na uchaguzi wake mwenyewe. Chuja upya chaguzi zako-**Young Killer Msodoki.**

# Kuumbe!

BONGO INGEKUWA VITA

## Rihana kwake burudani



INGEKUWA hapa Bongo, basi mitandao ingetawala matusi na maneno ya kashfa kutoka kila upande, kisa tu msanii fulani kafanana na mtu ambaye hana mbele wala nyuma.

Kuna baadhi watamtetea mlengwa kuwa kafanana naye sura, huku wanaounda timu ya mshidani husika wanakuja juu kwa kukataa katakata na kufikia hata kumdhalilisha Yule anayeidaiwa kufanana naye.

Hayo yalitokea kwa msanii Harmonize na kijana Harmorapa, kwani licha ya kufanana sura lakini wapo waliowatofautisha na wengine kufikia hatua ya kumdhalilisha na kumfananisha na mnyama pori.

Hiyo ndio hali ya Bongo, msanii mkubwa hawezi kufanana hata kidogo na kijana wa Manzese au Mbagala. Wanachokiamini Mungu hawezi kuumba mtu mwenye sura nba wajihi kama wake, na endapo akitokea basi ni vita kubwa.

Lakini kwa mwimbaji wa Marekani, Rihanna hali ni tofauti, yeye amediriki kuweka kwenye akaunti yake ya Instagram picha ya binti mdogo anayefanana naye sura huku akitamka wazi kwamba amefurahi kuona jambo hilo.

Picha hiyo imeonekana kusambaa kwa kasi kubwa siku ya July 24,2019 hukuRihanna akiwa ameandika caption iliyosomeka “Nusu niangushe simu yangu, kivipi?” ,

Baada ya kuweka posti hiyo, komenti zimekuwa nyingi na kila mtu ameandika wazo lake kuhusiana na picha hiyo ambapo wengine kuhisi kuwa huenda Rihanna akawa na undugu na mtoto huyo kutokana na wawili hao kufanana.

Mpaka sasa picha hiyo ina jumla ya likes milioni 6.3 na comments elfu 79 ndani ya saa 15 tokea ipostiwe kwenye ukurasa halali wa mwimbaji huyo na kutajwa kuwa ni miongoni mwa picha ambazo zimeingia kwenye rekodi ya kuwafikia watu wengi kwa muda mfupi.

Mwaka 2017 Beyonce alivunja rekodi ya kupata likes Milioni 6.3 ndani ya saa 8 baada ya kupost picha aliyotangaza juu ya ujauzito wake wa watoto mapacha na kumpiku Selena Gomez ambaye alishikilia rekodi ya likes Milioni 6.3 kwenye picha aliyoipost June 25 2016.



## Wakung’uta ’rhythm’ wanaokimbiwa Bongofleva



**Na Adam Fungamwango**

KATIKA muziki wa laivu ili uwe bora kunatakiwa kuwa na magita matatu au manne.

Hayo ni ‘solo’, ‘second solo’ au Wakongomani wanaliita ‘mini solo’, ‘rhythm’ na ‘bass’.

Ili muziki uwe bora na asikike vizuri kwenye masikio ya msikilizaji, unatakiwa uwe na idadi hii ya magitaa.

Lakini kama yatapungua na kuwa matatu, basi gitaa linalotakiwa kupungua hapo ni ‘second solo’.

Yaliyobaki matatu ni muhimu mno kwenye muziki wa dansi, na kama likikosekana moja hata ambaye hajui muziki anaweza kuhisi kuwa haijakaa sawa, au kuna mapungufu fulani.

Leo tunaaangalia wapiga magitaa ya ‘rhythm’ ambao kwa sasa ni kama hawapewi umuhimu sana, lakini kwenye miaka ya nyuma chombo hicho kilikuwa maarufu mno na wapigaji wake kuwa maarufu.

‘Rhythm’ ni gitaa ambalo linasaidiana na gitaa ongozi la solo, na ndilo linaloongoza muziki mzima.

Ndilo linaloongoza njia mzima ya wimbo husika kwa waimbaji wa wapiga vyombo.

Zamani kuna wakati linaachiwa dakika moja au mbili na kusikika vizuri mno, lakini kwa sasa si hivyo tena, lakini husikika kwa chini kidogo wakati wimbo unaendelea.

Cha ajabu ni kwamba wasanii wa bongo fleva, pamoja na siku hizi baadhi kutumia gitaa la solo, lakini hakuna anayekumbuka kutumia gitaa hilo. Na kama akitokea, basi anaweza kuleta utofauti mkubwa wa muziki wake kutokana na gitaa hilo kuwa na sauti inayosisimua na kuamsha hisia ya mwanadamu ndani ya moyo wake. Wafuatao ni wapiga magitaa ya ‘rhythm’ maarufu nchini.

**1. ABDALLAH GAMA**

Ni mpiga gitaa la rhythm bora kabisa kuwahi kutokea kwenye ardhi ya Tanzania. Umaarufu wake hasa umetokana na nyimbo nyingi alizopiga akiwa na DDC Mlimani Park Orchestra.

Kabla ya hapo aliwahi kupigia bendi za Safari Trippers, Dar International na alipotoka Sikinde alikwenda kupigia bendi ya Bima Lee. Gama bado yupo na anaendelea na muziki.

**2. MUSTAPHA HAMISI ‘PISHUU’**

Baada ya kuondoka kwa Abdallah Omari ‘Dulla’ aliyekumbwa kwenye wimbi la wanamuziki mwenda Sikinde, Msondo ilimtafuta mpiga rhythm bora bila mafanikio.

Lakini kwa mastaajabu ya wengi walimpata kijana mmoja Mustapha Hamisi, ambaye aliliziba kikamilifu na kuwa mmoja wa wapiga rhthm bora kabisa kuwahi kutokea nchini Tanzania.

Mashabiki wa Msondo wanampachika jina la ‘Pishuu’ wakimfananisha na mpiga rhythm mmoja wa bendi ya Shamashama ya nchini Congo DR mwenye jina hilo.

**3. MWARAMI SAID ‘GOLDEN FINGER’**

Sikinde ilibahatika kumpata mpiga rhythm mmoja matata sana aitwaye Mwarami Said, na mashabiki wakamuongeza jina lingine akawa ‘Golden Finger’.

Walimchukua kutoka kwenye bendi ya JKT Kimbunga Stereo. Huyu hakuwa mahiri kwenye upigaji tu, lakini alikuwa mkali kwenye kutunga nyimbo pia.

Akiwa na Kimbunga, alitunga wimbo wa ‘Majambazi’ na ‘Rumba Kimbunga’. Akiwa Sikinde alitunga nyimbo nyingi zikiwemo zile maarufu za ‘MV Mapenzi namba mmoja na mbili. Sasa ni marehemu.

**4. KASSIM KARUONA**

Bendi ya Tabora Jazz ilikuwuwa mahiri mno kwa staili yake ya kupiga muziki halafu unazimwa na kuachiwa mpiga rhythm pekee na drums wakihenyeshana.

Kassim Karuona alipata umaarufu mkubwa kwenye bendi hiyo kutokana na uhamiri wake mkubwa wa kupiga gitaa hilo. Ukiangalia hata wimbo wa ‘Dada Asha’ ulirudiwa na bendi maarufu ya Congo, Soukouss Stars, lakini mpiga rhythm wao maarufu Lokassa wa Mbongo hakuweza kufikia ubora ya ile rhythm asili iliyopigwa na Karuona kwenye ‘Dada Asha Original.’

**5. ALLY SAID**

Moja kati ya wapiga magitaa ya ‘rhythm’ ambao historia ya muziki wa Tanzania haimtedei haki ni Ally Said.

Hatajwi sana na wachambuzi wa muziki na mashabiki, lakini ukisikiliza nyimbo nyingi alizopiga utagundua kuwa hana mfano wake.

Nyimbo nyingi za Urafiki Jazz kuna vipande vimeachiwa gitaa la rhythm litambae na yeye ndiye aliyepiga nyimbo nyingi kama ‘Asma’, ‘Paulina’, ‘Unguja na Tanga’, ‘Mauji wa Soweto’, Rudisha Pete Lucy’ na nyingine ambazo amepiga kwa ustadi mkubwa.

Kabla ya hapo alikuwa kwenye bendi ya Cuban Marimba na TK Limpopo. Nyimbo za ‘Maisha ya Sasa’, ‘Subisubi’, zinathibitisha bila shaka uwezo wake.

Mpigaji maarufu wa gitaa la Rhythm nchini Congo DR miaka ya ‘70 hadi mwanzoni ‘80 Vata Mombasa ambaye kwa sasa anaishi nchini Ivory Coast. Huyu ndiye mwasisi wa staili au upigaji ambao ulifuatwa na kuigwa na wapiga magitaa hayo wote nchini wakiwemo walioorodheshwa hapa.

Hizi ni picha zake mbili moja ikiwa kwenye miaka ya ‘70 kwenye kilele chake cha mafanikio na ya pili ya miaka ya hivi karibuni

# Vijimambo

## PICHA ILIYOPITA



1. Wanasema eti mimi chizi. Watanzania bwana kwa figisu! - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
2. Duuh! Jamani kazi kwanza, kuselifika baadae - Bahati, Kiwalani DSM.
3. Hii mitandao ya kijamii inatutesa. Kwa hii selfii kila mtu atakomenti 'nice' - Agatha Mbale, Moro Town.
4. Natafuta picha ya kutupia 'whatsap' - Dullah Dimoso, Tabata DSM.
5. Kijana hiyo simu imepitwa na wakati, ipeleke makumbusho - Oiso, Nyaishozi Tegeta DSM.
6. Ukisikia uchizi taslimu, basi ndio huo. Simu ya mezani na selfii! - Mama Nah, Manzese DSM.
7. Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.
8. Yes, hapa sasa pozi limekubali, ngoja nijifotoe sasa - Samwel Sungi, Utemini Singida.
9. Hii simu vipi, mbona sioni sehemu ya kujiselfisha? - Msabaha J. Msabaha, Mikindani Mtwara.
10. Lazima baby wangu aikubali hii picha, si selfii ya kitoto - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
11. Hii inaitwa 'ekotite', muulizeni Kofi Olomide anaifahamu sana - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
12. Kweli ushamba mzigo. Wewe, sio kila simu unaweza kujiselfisha nayo - Mariam Beneali, Migombani Zenji.
13. Ha ha haaa, usitake ncheke mie! Hebu rudisha simu ya watu ofisini - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
14. Hapo 'chacha'! Disco limeingia watu wa kabila lileee! Mtajuta kuijua selfii - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
15. Mnashangaa nini? Mie sijiselfishi kama nyie, mie fundi simu jamani - Dully, Kiembesamaki Zenji.
16. Ukitaka kugombana naye, mwambie kuwa hiyo simu haiselfishi - Antar, Makumbusho Kijitonyama DSM.
17. Hapa sasa mademu wote wa 'bush stars' wangu - Nahoja Mazengo, Mbande Chamazi DSM.
18. Wewe! Hebu acha ushamba wako bwana, unawaabisha Wairinga wenzip - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
19. Hiyo selfii yako inanitia homa kwa kicheko - Bimkubwa Ausi Juma, Michenzani Unguja.
20. Hilo ndio tatizo la Wahehe wakishaingia mjini - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
21. Kaa hivyo hivyo, baada ya 'masaa' kadhaa utaona sehemu ya kupigia picha inajionyesha - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
22. Watu wa kizazi hiki, kweli wamedata. Haya bhana na selfii yako bandia - Mama Nah, Manzese DSM.
23. Kweli ushamba zigo la miba. Tangulini simu hiyo ikatumika kwa selifii? - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
24. Hiyo ni sawa na kuosha mchele kwenye mto wa maji mengi. Utapata taabu sana - Semeni Mpanjira, Kilwa.

**SMS Bomba ya Leo:**
**Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.**

## PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0773 477 311**




# Mwachumvi: Mgaagaa na upwa hali wali mkavu

**Na Adam Fungamwangwo**

WASWAHILI wana msemo 'Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.'

Tafsiri yake kwa kiswahili kinachoeleweka vizuri ni kwamba mtu anayezungukazunguka pwani ya bahari, basi huwa hakosi kitoweo.

Ina maana hata kama hajui kuvua, lakini anaweza kupewa au kuzawadiwa samaki kutoka kwa wavuvi.

Mara nyingi wavuvi wakishafika pwani wanachagua samaki wanaowataka wao, lakini wengine wanawagawa kwa watu mbalimbali wanaokuwa ufukweni. Hivyo yoyote ambaye anayependa kutembelea hapo, hakosi kurudi nyumbani na kitoweo.

Tukirudi kwenye maana na ni kwamba mtu yoyote anayetoka kwenda kutafuta huwa hakosi chochote, ni tofauti na mtu anayekaa tu nyumbani. Hii inafana na ile ya 'mtembea bure si sawa na mkaa bure'.

Hali kama hii inajitokeza kwenye filamu ya 'Mwachumvi'. Wahusika kwenye filamu hii ni Ali Kalawi, Haji Mboto, Luckey Lukamo, hayati King Majuto, Muhogo Mchungu, Anita Sudi, Mau Chiwaga, Sabrina Paul na wengineo.

Anaanza kuonekana Mzee Majuto na kijana wake Kalawi wakizungumza. Majuto anampa siri mwanaye kuwa hana uhakika na binti yake Mwachumvi kama ni mtoto wake kweli au amebambikiwa.

Anamwambia Kalawi kuwa wakati akiwa mdogo, alikuwa na uhusiano na mwanamke mmoja kijiji cha jirani. Lakini baadaye akawa mjamzito. Huko huko kijiji jirani alikuwa na bwana mwingine, hivyo alipoambiwa hivyo akaukataa ujauzito.

Hata hivyo alipojifungua, binti huyo alikuja kumbwagia mtoto akiwa bado mdogo na yeye kutokomea kusikojulikana. Akasema ilileta ugomvi kwa mama yake Kalawi, lakini baadaye akakubali kumlea, hadi mama huyo alipofariki.

Kutokana na hali hiyo akamwambia kijana wake kuwa asimwambie lolote dada yake kuhusu jambo hilo, kwani hajui chochote, anachojua yeye ni kwamba marehemu mama yake Kalawi ndiyo mama yake mzazi.

Kalawi akamuahidi baba yake kuwa hatofanya hivyo. Lakini pamoja na



hayo, Majuto alionekana kumtenga Mwachumvi kimasomo kwa sababu hakumpeleka shule.

Kijijini hali inakuwa mbaya. Kalawi hana kazi na dada yake kutwa kutembea na mabwana ambao hawana nyuma wala mbele. Kalawi alionekana kumpenda sana dada yake na hakutaka aharibike kimaisha. Akamshauri wakimbilie Dar. Mze Majuto aliwakatalia kata kata. Lakini wakatoroka.

Dar kama kawaida ikawapokea. Chumba kimoja nyumba ya kupanga ikawa ndiyo makazi yao.

Aina yake ya maisha ya kulala chumba kimoja mtu na kaka yake ilisababisha watu wawafikirie vibaya. Walichokila na kukivaa wanakijua wenyewe. Wakipata wanakula, wakikosa wanalala.

Misukosuko wanayoipata, wanampigia simu baba yao Majuto kuomba walau auze kipande cha shamba na kuwatumia pesa. Majuto alikataa kwa sababu walimtoroka, hawakumuaga.

Kalawi akawa anafanya kazi ya kusafisha magari. Moja yagari lilikuwa na la Mboto, kijana aliyekuwa ana kazi na kipato kizuri. Kalawi anamhadithia maisha yake jinsi yalivyo. Haji anaingiwa na huruma na kwenda kuangalia wanapoishi. Anamkuta binti mmoja mrembo Mwachumvi. Mate yakamvuja.

Urafiki wa Mboto na Kalawi uliendelea, lakini baadaye ukageuka ushemeji kwa sababu Mboto alimhitaji dada yake. Kalawi anakwenda kumwambia dadaye akubali kuolewa na Mboto.

Pamoja na matatizo mengi ya hapa na pale, ndoa inafanyika, Mwachumvi anaolewa na kijana mwenye pesa, Mboto.



KAPAGAWA

# Card B amchizisha Offet

UNAWEZA kusema mapenzi sawa na uwendawazimu! Mara nyingi mtu akipenda sawa na kipofu, kila kitu kwake ni kitamu na pale inapotokea hitilafu na kukaa kando kidogo ni rahisi kurudi haraka.

Hivyo ndivyo inatokea kwa wasanii maarufu nchini Marekani, rapa Card B na mpenzi wake Offset, ambao miezi michache ya kutengana hivi sasa wamerudiana na kuonyesha mapenzi motomoto.

Hali ya mahaba niue imekuja siku kadhaa tokea Cardi B na Offset kutangaza kurudiana baada ya wawili hao kutengana mwishoni mwa mwaka jana 2018.

Katika kuonesha amepagawa na wengine kuona kama uwendawazimu wa mapenzi, mrembo huyo ameonekana kumkoleza mume wake huyo kwa kuchora tattoo lenye jina la 'Offset' nyuma ya paja lake.

Imeelezwa kuwa Offset pia alishawahi kuchora tattoo yenye jina la Cardi B kwenye shingo yake ikiwemo majina ya watoto wake wote wanne na watu wake wa karibu anaowapenda.

Hata hivyo mashabiki hawakumuacha hivihivi, walimpa maneno ya shombo na kumwambia mapenzi hayo ni sawa na kung'arisha dhahabu ya kale.

Wengine walihoji huenda Cardi B amefanya hivyo kurudisha upendo ambao Offset amekuwa akimuonyesha ikiwemo na kuchora jina lake tattoo.

Wanaowaunga mkono walisema kuwa mapenzi hayo yanayoanikwa hadharani ni halisi na ya dhati yanayomsukuma Cardi B kufanya hivyo.

# Yeti, Tacha warudishwa BBNaija



WASHIRIKI wa shindano la BBNaija Seyi na Tacha ambao waliondolewa ndani ya nyumba kimakosa wamerudishwa kuungana na wenzao.

Seyi na Tacha waliingia ndani ya nyumba hiyo siku ya Jumanne ya wiki hii saa moja usiku na kuamsha shangwe kwa washiriki wengine.

Kabla ya kuingia, kiongozi wa BBnaija alisema Seyi na Tacha walikuwa wahanga wa wanaoondolewa hewa na kwamba bado wanaendelea kupigania zawadi nono ya shindano hilo.



## Davido wewe noma

MWANAMUZIKI mkali, Davido, ametajwa kuwa ndiye mtu tajiri zaidi kwa wafuasi wa mtandao wa Instagram nchini Nigeria.

Kwa mujibu wa mtandao wa Hopper HQ, katika orodha iliyotolewa mwaka 2019 akaunti ya Davido imefikia thamani ya Naira milioni 26 na kushika nafasi ya pili kwa Afrika.

Wasanii wengine walioingia tano bora ni Funke Akindele Bello, Ayodeji Balogun aka Wizkid na Tiwa Savage.

## Genevieve ulichokifanya Mungu anakuona

WASANII wengi nchini Nigeria wamemjia juu mkongwe wa filamu, Genevieve Nnaji, baada ya kuposti picha ikimuonyesha akiwa na mavazi yaliyomuacha nusu utupu.

Kama vile haitoshi baadhi ya wasanii na mashabiki wamehoji kama mwigizaji huo aliyejizolea umaarufu kama alifanya uamuzi sahihi kuachia picha hiyo hadharani.

Waliojitokeza kupaza sauti ni Funke Akindele, Uche Jombo, Ini Edo, Toyin Abraham, Richard Mofe-Damijo na mashabiki wengine.





## Meneja: 'Sitomwacha R Kelly peke yake'

DARRELL Johnson amekanusha vikali kwamba hakupata faida binafsi kutokana na kazi yake ya kusimamia mgogoro wa R.Kelly.

Meneja huyo anayeshughulikia mgogoro wa mwanamuziki R.Kelly, amesema hakufukuzwa kutoka katika timu yake ya kisheria kufuatia taarifa aliyopewa na kueleza hatamwacha binti yake na mtu anayemtuhumu.

Wakati akizungumza na TMZ, Darrell Johnson alisema aliamua kuchukua mapumziko kutoka kwa timu ya kisheria ya R.Kelly kama dharula kutokana na mtoto wake kuwa mahututi hospitalini.

## Jada kweli unajua kupenda

MAMA wa mto wato mwanamuziki Wizkid, Jada Pollock , ameibuka na kudai akaunti yake ya Instagram ilidukuliwa na watu wasiojulikana.

Jada aliamua kutoa kauli hiyo baada ya hivi karibuni kuibuka majadala baada ya kuonekana akilalamika kuhusu unyanyasaji anaofanyiwa na mwanamuziki huyo maarufu Afrika.

Mrembo huyo ambaye amezaa mtoto wa tatu wa Wizkid amesema hawajibiki kwa tuhuma hizo kwani watu wasiojulikana waliiteka akaunti yake na kudukua taarifa zake muhimu.



SAFU

## MIONZI YA SHERIA



Na John Juma
0716217615

# Ijue haki ya notisi kwa mpangaji

KUNA matatizo jamii kati ya wapangaji na wenye nyumba, kuhusu notisi ya kuondoka au kuondolewa katika nyumba. Wako wanaosema notisi ni ya mwezi mmoja, pia wako wanaosema ni ya miezi mitatu. Kama ni kweli au vinginyevyo, tuone sheria husika inasemaje?

Masuala ya pango yanaongozwa na sheria kuu mbili. Moja Sheria ya Ardhi Namba 4 ya mwaka 1999; pili Sheria ya Mikataba Sura ya 345. Kwa pamoja sheria hizo zote kwa mapana, husimamia jambo husika.

**MKATABA WA PANGO**

Mkataba wa pango, unahusisha makubaliano ya upangaji kati ya mwenye nyumba na mpangaji au mpangaji na mpangaji mwingine wa pili. Pango linaweza kuwa kwa ajili ya chumba/nyumba ya kuishi, biashara, nyumba ya ibada au hata shughuli nyinginezo za kibinadamu. Yote hayo, kwa ujumla ndiyo yanayokamilisha maana ya neno pango.

Aina za mikataba

Sheria ya Ardhi, 1999 (Kifungu cha 78 na 79) inatambua mikataba ya upangaji ya muda mrefu na kwa vipindi vifupi. Inatambua pango la wiki, mwezi, miezi, mwaka na miaka. Imetoa uhuru kwa wahusika wenyewe kuamua ni muda gani wangependa kuingia mkataba.

Katika vitu muhimu sana katika suala la pango, ni notisi ya kuondoka au kuondolewa katika pango. Jambo la kuzingatia awali kabisa, ni kuwa notisi hii ni muhimu pande zote mbili.

Upande wa mwenye nyumba na upande wa mpangaji. Kila mmoja kwa nafasi yake anawajibika kutoa notisi kwa mwenzake, penye mahitaji ya kuondoka au kuondolewa.

Ikumbukwe kuwa, notisi si kwa ajili tu ya kuondoka na kuondolewa, bali yanapotokea mabadiliko yoyote katika masharti ya mkataba. Hiyo ina maana kwamba, hata kuongeza kodi, kupanga kukagua nyumba, kufanya marekebisho, notisi inaaa itolewe.

Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999 haijatamka moja kwa moja kuhusiana na suala la notisi ya kuondoka au kuondolewa iwe ya muda gani. Kinachohitajika na cha muhimu au lazima, ni kuhakikisha notisi inatolewa katika muda unaokadirika na kuingia akilini, wataalamu wa sheria.

Hivyo, notisi inaweza kuwa ya muda wowote isipokuwa uwe unaokadirika na kuingia akilini.

Ili kuenenda kiungwana, mhusika anafaa aangalie muda wa pango uliopo katika mkataba. Kwa mfano, mtu mwenye mkataba wa miaka mitano, hawezi kupewa notisi ya kuondoka ya mwezi mmoja au hata miwili.

Lakini, kwa mwenye mkataba wa miezi minne au mitatu, anaweza kupewa notisi hata ya mwezi mmoja. Hali kadhalika, wa mwaka, notisi ya miezi mitatu inaweza kuwa sahihi.

Muhimu ni Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999, haijataja wazi wazi muda hasa wa notisi ya kuondoka, hivyo ni vyema sana kuhakikisha mkataba wa pango unaeleza muda wa notisi.

Inalaezwa kwamba, ni muhimu sana, endapo muda utafika mwenye nyumba anataka chumba au nyumba yake au ikiwa mpangaji anahitaji kuondoka.

Kwa mujibu wa makubaliano yaliyopo, muda wowote wahusika watakaokuwa wamekubaliana unatosha na unakubalika kisheria, kwa sababu unatokana na hiari za wahusika.

Isitoshe, mhusika asikubali kusaini mkataba ambao hauelezi muda wa notisi. Hatua hiyo itamwepusha na masahibu ya baadaye.

Tabia hiyo ni kosa kwa mujibu wa taratibu za kisheria, hususan ile ya mikataba: Kifungu cha 73 (1), inasema ikitokea hivyo, basi mwenye nyumba lazima atawajibika kumlipa fidia mhusika, yaani mpangaji wake.

Ni kosa ama kuvunja au kusitisha mkataba wa pango kama ilivyo kuvunja mikataba mingine yoyote kinyume na taratibu za sheria.

Mwisho, jambo hilo ni tofauti kidogo, na pale mpangaji anapoamua kuondoka yeye mwenyewe katika chumba/nyumba kabla ya mkataba kwisha. Mwenye nyumba hatowajibika kwa chochote au lolote lile, zaidi labda akifanya ni uungwana tu. Naomba kuwasilisha.

## KALAMU YA MWALIMU



Na Reubeni Lumbagala

# Waombaji wa elimu ya juu wanahitaji umakini mkubwa

SIKU ya 15 Julai iliyopita, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ilifungua pazia kwa waombaji kuomba nafasi mbalimbali katika vyuo vilivyopo nchini ili kuweza kujiunga kusomea kozi wazipendazo, ili kutimiza ndoto na malengo waliyojiwekea.

Kazi ya uombaji huo wa nafasi za vyuo vikuu linaendelea hadi Agosti 10, 2019 litakapohitimishwa kwa awamu ya kwanza. Hii ni fursa adhimu kwa vijana waliohitimu kidato ch sita mwezi Mei mwaka huu na wale wanaopenda kujiunga na elimu ya juu kuchangamkia fursa hiyo haraka.

Kutokana na unyeti wa kozi zinazotolewa na vyuo vikuu, ni muhimu kwa waombaji wa kozi hizo kufanya tafakuri pana kabla ya kuingia katika mfumo na kuanza kuomba kozi kwani kozi hizo ni safari ya kutimiza hatima zao kupitia elimu watakayoipata vyuoni.

Waombaji wa kozi za elimu ya juu wanapaswa kuzingatia yafuatayo kwa umakini mkubwa. Mosi, mwombaji atambue aina ya kazi anayopenda kufanya baada ya kuhitimu masomo yake.

Kwa kutambua aina ya kazi anayopenda kuifanya baada ya kuhitimu elimu ya juu, utakuwa mwongozo wake wa kutambua aina ya kozi ya kusomea.

Mathalani, ikiwa mwombaji anapenda kufanya kazi ya uhasibu. Kozi zitakazomfaa hapo mwombaji anajumuisha maendeleo kama shahada ya uhasibu, usimamizi wa fedha na biashara.

Pili, mwombaji aliunganishe kiwango cha ufaulu wake na sifa za kozi anayotaka kuomba kama zinaendana.

Ni vyema mwombaji akafahamu kiwango cha ufaulu kinachohitajika kwa waombaji wa kozi husika, ili alinganishe ufaulu wake kama unakidhi sifa zilizoainishwa. Ikiwa mwombaji atakuwa na ufaulu ambao ni chini na kiwango kinachohitajika katika kozi anayopenda kuomba, anapaswa kuacha kuchagua kozi hiyo na kuchagua nyingine inayoendana na ufaulu wake, ili apate sifa stahiki za kuchaguliwa.

Kwa mfano, kozi ya shahada ya kilimo, ikihitaji mwombaji aliye na ufaulu wa daraja la kwanza au la pili. Mwombaji mwenye ufaulu wa daraja la tatu, hapaswi kuomba kozi hiyo, kwani anakuwa amekosa sifa za kuchaguliwa kwa kutokukidhi kiwango cha ufaulu husika.

Ili kuepuka kukosa kabisa nafasi ya chuo, mwombaji mwenye daraja la tatu, anashauriwa kuomba kozi zinazohitaji ufaulu wa daraja la tatu ili kuchaguliwa na si kukosa kabisa nafasi ya chuo.

Tatu, mwombaji aombe kozi zenye uhusiano na mchepuo (combination) aliyosomea. Vyuoni zipo kozi nyingi zinazoendana na tahasusi za sayansi, sanaa, biashara na kilimo.

Tahasusi hizi zote zina kozi zinazoendana nazo kwa waombaji wa vyuo vikuu. Mathalani, mwombaji aliyesomea masomo ya sanaa, anaweza kusomea kozi kama vile, ualimu wa masomo ya sanaa; uandishi wa habari, sheria, utawala, maendeleo ya jamii, uhusiano wa kimataifa, sayansi ya siasa, au mazingira.

Aliyesomea sayansi anaweza kusomea kozi za uhandisi, famasia, udaktari, kilimo, mifugo, mimea. Kozi zinazoendana na masomo ya biashara, ni pamoja na uhasibu, masoko, uchumi na huduma za fedha.

Hivyo basi, itakuwa ajabu kwa mwanafunzi aliyesomea sayansi kuomba kozi za uandishi wa habari, maendeleo ya jamii, sheria nk, kwani kwa kufanya hivyo atakuwa amejikosesha nafasi yeye mwenyewe kwani mwombaji huyo alipaswa kuomba kozi zinazoendana na elimu ya sayansi aliyosomea kidato cha tano na sita au katika ngazi ya stashahada.

Nne, mwombaji aombe chuo chenye aina ya kozi aitakayo. Hili ni jambo la msingi sana kuzingatiwa na waombaji wote. Kabla mwombaji hajaomba nafasi ya kujiunga na elimu ya juu, ni vizuri afanye utafiti wa vyuo vinavyofundisha kozi azipendazo, ili atakapoingia mtandaoni kuomba nafasi za kujiunga katika vyuo mbalimbali, azingatie kuomba vyuo vyenye kutoa kozi zinazoendana na matakwa yake.

Kwa kushindwa kufanya hivyo, mwombaji anaweza kupoteza nafasi kwa kudhani kozi zake hazipatikani katika vyuo na hivyo kughairi kufanya maombi.

Tano, mwombaji anapaswa azingatie kupangilia kozi anazopenda kuzisoma kwa mtiririko mzuri. Katika kuomba kozi, mwombaji aanze na kozi anayoipenda zaidi kwa kuiweka namba moja ndipo kozi nyingine zifuate kwa mujibu wa matakwa yake.

Endapo mwombaji ataomba kozi bila kupangilia mtiririko, atajikuta akichaguliwa kozi ambayo si chague lake namba moja na hivyo kujikuta akisoma kozi ambayo si kipaumbele chake.

Kama mwombaji anapendelea kusomea kozi ya sheria au utawala, ahakikishe kozi ya sheria anaiweka namba moja ikifuatiwa na kozi ya utawala. Ikiwa mwombaji ana sifa zote za kukidhi kuchaguliwa kozi aliyoiweka namba moja, basi moja kwa moja yuko katika nafasi nzuiri ya atachaguliwa kusomea kozi hiyo.

Kwa haya machache, yanaweza kuwasaidia waombaji wa kozi mbalimbali za elimu ya juu. Uombaji wa vyuo unaendelea. Nawasihi waombaji waitumie fursa hiyo kabla ya tarehe 10, mwezi ujao litakapofungwa kwa awamu ya kwanza. Tafakari.

KUELEKEA UCHAGUZI MTAA DODOMA

# KAMANDA TAKUKURU: TUN WAO TUTAKAOWANASA K

■ Wapigaji, wagombea washangilia mafunzo

**Na Renatha Msungu, Dodoma**

ILI kuhakikisha kunafanikishwa lengo la kuwapata viongozi bora wa serikali za mitaa katika uchaguzi wa wenyeviti wa serikali za mitaa, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imeanza kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na namna ya kuepuka upokeaji rushwa kwa wagombea katika nafasi mbalimbali.

Uchaguzi wa serikali za mitaa unatarajia kufanyika Oktoba mwaka huu na tayari wagombea wa nafasi hizo wamesimama kuwania nafasi wanazodhamiria.

Elimu hiyo, hivi sasa inatolewa na taasisi hiyo kupitia mafunzo na kongamano mbalimbali zinzofanyika katika maeneo tofauti jijini Dodoma, chini ya uratibu wa Takukuru mkoani humo.

Kama ilivyo sheria inayoundwa chombo hicho, awali iliundwa katika sura ya kupambana na rushwa na ndio maana iliitwa Taasisi ya Kupambana na Rushwa, lakini baada ya mapitio ya kisheria, ikawa Takukuru, ikiwa na jukumu la kuanza kuzuia ndipo inapambana pale inapobidi.

Hapo vinatumika vipeperushi vilivyoandaliwa taasisi, vikifafanua madhara ya kupokea rushwa kutoka kwa wagombea.

Hivi sasa jijini Dodoma, kampeni hizo zimepamba moto Takukuru, katika maeneo tofauti ya jiji hilo, maofisa wake wakitembelea maeneo ya elimu kama vile shule za msingi na sekondari, pia vyuo vikitoa somo kwa vijana wanaowaingiza masomoni.

Pia, kupitia mustakabali huo, jamii nayo katika sura ya pili inaonekana kuelewa somo hilo kwa kasi ya kuridhisha.

Kinachofanywa na Takukuru hivi sasa, ni kwamba inajikita katika kusambaza wadau watoa elimu hiyo kila pembe ya Jiji la Dodoma, ili kuhakikisha ujumbe unawafikia vilivyo.

**ELIMU ILIKOJIKITA**

Sosthenes Kibwengo, ni Kamanda wa Takukuru Mkoa wa Dodoma, anayesema kwamba wameamua kutoa elimu hiyo kwa jamii, kwa sababu taifa linahitaji kupata viongozi bora kuanzia ngazi ya chini hadi taifa, ukiwa ni msingi wa kuiletea jamii maendeleo.

Kibwengo anaeleza kuwa umuhimu wa elimu hiyo kwa watu wa rika zote, kwa sababu inawasaidia kuelewa madhara ya kuchagua viongozi wanaopatikana kupitia milango ya rushwa, kwani ina utamaduni wa kuwagharimu wananchi baada ya muda.

Anafafanua zaidi kuwa, taasisi hiyo imeona vyema kuanza kutoa elimu hiyo, ikiwamo katika mtazamo wa kusisitiza wananchi kujua madhara ya rushwa katika kipindi cha uchaguzi na kipindi nje ya uchaguzi, wanapoendesha maisha yao ya kila siku.

"Takukuru Dodoma tumejipanga vilivyo kuona makao makuu inapata viongozi waadilifu watakaochaguliwa kihalali na si vinginevyo," anasema.

Kibwengo anasema, hakuna sababu ya wakazi wa maeneo mbalimbali kurubuniwa na rushwa ndogo, ambayo ina sura ya kuwagharimu pale watakapochangua kiongozi batili, anayeingia katika nafasi kwa nguvu ya pesa.

Rai yake Kibwengo ni kwamba, wananchi wazingatia maudhui na maelekezo ya elimu hiyo wanayopewa kutoka Takukuru, mkoani Dodoma na kwingineko nchini, ili iwasaidie katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika hivi karibuni.

Anasema, hatua waliofikia sasa wamekwishatoa elimu hiyo katika shule ya msingi na sekondari za wilayani Bahi na Dodoma Mjini na wanaendelea na kutoa elimu hiyo kwa jamii, kuhakikisha walengwa wote wanafikiwa.

Kamanda huyo anasema, wahisika wakuu wanaoguswa moja kwa mpoja ni wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi huo wa serikali ya mtaa.

Anaeleza mbinu inayotumika katika mustakabali huo, ni kupitia mikutano ya hadhara inayofanyika katika maeneo mbalimbali, husussani kwenye maeneo ya mikusanyiko ya watu wa aina tofauti.

"Hii elimu tunaamini imemgusa kila mmoja. Tunaendelea kutumia mikusanyiko na klabu zilizoanzishwa kwa ajili ya kutoa mafunzo ya madhara ya kupokea rushwa, ili umchague mtu fulani," anasema Kibwengo.

Kamanda Kibwengo anasema, wananchi kwa jumla wanapaswa kujua wajibu wao, kwa sababu wao ndio waathirika wakuu, kabla ya kufuata ngazi nyingine ya umma.

"Kila mwananchi ana wajibu wa kutambua kwamba hiki sio kipindi cha mavuno, kwa sababu hakuna sheria inayoruhusu mtu atoe rushwa ili ashinde nafasi anayogombea," anasema Kibwengo.

Pia anautahadharisha umma kwamba usikubali kurubuniwa na rushwa ndogo ambazo zinaishia katika kuwadhalilishwa, kwani katika hatua ya baadaye, wahusika ambao ndio wapiga




Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alipozungumza na wanahabari, kuhusu kampeni ya elimu kwa wananchi kupambana na rushwa wakati wa uchaguzi. **PICHA: RENATHA MSUNGU.**



Ofisa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Stephen Elisante, akimtazama msimamizi msaidizi wa uchaguzi jijini Dodoma, wakati wa mafunzo yao kwa vitendo walipojiandaa na uchaguzi mdogo wa ubunge na udiwani, uliofanyika Septemba 16, 2018. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

# NAANZA KWA ELIMU, OLE WA RUSHWA WAKATI HUO




kura na wanaowachagua viongozi, wanashindwa kumhoji aliyechaguliwa.

Kibwengo anatoa elimu hiyo, akitafsiri madhara ya rushwa inaanzia pale, wanakutana na kundi la watu kwa ajili ya kufanya maamuzi ambayo sio sahihi mbele ya jamii na inaishia katika kulipa taifa hasara kuu.

Mkuu huyo wa Takukuru Dodoma, anasema hilo linaishia katika taifa kupoteza rasilimali zake, ikiwamo miradi mkubwa ya maendeleo inayoendelea na ile iliyoanzishwa.

Kibwengo anasema, kiongozi atakayechaguliwa kwa nguvu ya fedha yake, iko wazo moja kwa moja anashindwa kuendeleza miradi hiyo ya umma, badala yake atahitaji kufanya awezavyo kurejesha kiasi cha fedha alichotumia wakati wa uchaguzi.

"Ndio maana tunasisitiza kutoa elimu kwa wananchi, jinsi ya kuepukana na rushwa," anasema Kibwengo, ambaye katika ufafanuzi wake, hachoki kuhimiza elimu kwa mpiga kura wake."

**USHAURI WAKE**

Kamanda Kibwengo katika ushauri wake anasisitiza kwamba hakuna sababu ya mgombea nafasi ya uongozi kuelekeza fikra zake katika rushwa, iwapo anajiamini.

Kikubwa katika ufafanuzi wake ni umakini katika kuandaa na kunadi sera na mwelekeo wake kisiasa, katika kushika nafasi ya uongozi anaowania kupitia kura za wananchi.

Tahadhari kuu ya kamanda huyo ni kwamba, kupitia elimu waliotoa kwa wananchi na wagombea kwa ujumla, ni haja ya umakini na iwapo kutakuwapo na ukiukwaji wa kanuni na sheria za uchaguzi kwa wagombea na wapiga kura, Takukuru haitakuwa na msamaha.

Anahimiza kuwa ukiukwaji wowote vyenye viashiria vya rushwa, mkondo wa sheria utachukua hatua, akitafsiri hilo ni 'uhujumu uchumi wa taifa.'

Kutokana na hilo, ushauri wake ni kwamba wagombea wa nafasi hizo wahakikishe wanajiandaa vizuri kabla ya uchaguzi huo na wasitegemee kuwarubuni wananchi, kwa sababu nafasi ya elimu wameshapewa na Takukuru.

Bosi huyo wa Takukuru anasema, hatua waliyochukua, ni msaada tosha katika uchaguzi, ikisaidia kupembua nani anafaa na asiyestahili kuchaguliwa.

**WAGOMBEA WALONGA**

Timu ya Takukuru ikiongozwa na Kamanda Kibwengo, wanajikita katika kujiamini katika azma ya kupitia nafasi wanayoenda kugombea, kwa sababu ni kazi wanayoijua na hakuna sababu ya kuendekeza rushwa katika kusaka nafasi ya kuchaguliwa.

"Takukuru imejiandaa kupambana na suala hilo. Kinachotakiwa, tumieni mbinu sahihi ambazo zimewekwa kushawishi watu wakuchague," anasema Kibwengo.

Pia kwa upande wa wananchi, wanakiri elimu ya rushwa waliopata kutoka Takukuru wakionyesha imani kwamba imesaidia kwa kiasi kikubwa kuwapa uelewa thabiti katika sura kuu kwamba 'siyo kitu kizuri.'

Hiyo inachukua mustakabali sana katika kipindi kilichoko kuelekea uchaguzi mkuu mwakani na ngazi ya serikali ya mtaa, ambayo vuguvugu liko juu zaidi.

Mnufaika wa elimu hiyo, Ismail Ally, anaahidi kwamba ataitumia elimu hiyo katika uchaguzi ujao, ili kuhakikisha anachagua viongozi bora wenye sifa zinazostahili na si anaowaita 'bora viongozi' wanaojilinda kwa kutumia fedha kuwarubuni wapigakura.

"Tunaishukuru Takukuru kwa kutupa elimu hii, kwa sababu naamini itasaidia sana kuchagua viongozi bora wasiotoa rushwa," anaongeza Kibwengo.

**WANASIASA JE?**

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Chinyoyo, iliyoko katika Kata ya Kilimani, jijini Dodoma, Faustina Bendera, anasema Takukuru mkoani Dodoma imefanya jambo zuri kutoa elimu sahihi dhidi ya rushwa kwa jamii, kwa sababu anaamini itawasaidia kwa kiasi kikubwa wananchi.

Anafafanua kwamba, inakuwa msaada unaowezesha kumwelewa kiongozi anayepaswa kuchaguliwa, tofauti picha iliyozoeleka awali.

Faustina anasema, elimu ya rushwa hivi sasa inatolewa na Takukuru kwa wananchi kila kona, jambo linalowajenga na kuwaweka katika hisia kwamba, hawatakubali kupewa rushwa na baadhi ya wagombea katika ngazi kama ya khanga na tisheti kumwingiza katika uongozi.

"Sasa hivi tunaamini, katika uchaguzi huo hakutakuwapo nguvu ya pesa, kwa sababu wananchi wamepata elimu kutoka Takukuru tuna imani watachagua viongozi bora na si bora viongozi," anasema Faustina.

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 10 00)

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | | 4 | | ■ | 5 | ■ | 6 | 7 | | |
| 8 | | | ■ | | ■ | ■ | 9 | 10 | | | ■ | ■ |
| 11 | | | 12 | | ■ | 13 | | | | | | ■ |
| | ■ | 14 | | | | | | | ■ | | ■ | 15 |
| 16 | | | | | ■ | 17 | | | | | | |
| | ■ | 18 | | | 19 | | | ■ | ■ | | ■ | |
| | ■ | 20 | | | | | ■ | 21 | | | | |
| | ■ | ■ | | ■ | | ■ | ■ | | ■ | | ■ | |
| ■ | ■ | 22 | ■ | 23 | | | 24 | | 25 | | ■ | |
| 26 | ■ | | ■ | ■ | | ■ | 27 | | | ■ | ■ | |
| 28 | | | | | | ■ | 29 | | | | 30 | |
| | ■ | | ■ | ■ | ■ | ■ | | ■ | | ■ | | ■ |
| | ■ | ■ | 31 | | | | | | | ■ | | ■ |

Dondoo: Kulia

1. Nchi ya pili kwa ukubwa duniani 6. Rukia ghafla 8. Kwepa 9. Toka sehemu moja hadi nyingine 11.Pesa ya Nigeria 13.Wingi wa neno mdudu 14.nguruma 16.Nabii wa Mungu 17.Waziri mkuu mpinzani Uganda 18.hufunga na kufungua 20.Tangazo 21.Makazi ya watu wengi 23.Mavu, nyigu 27. Ami 28.Jiji la pili kwa ukubwa nchini 29.Kipawa 31.kazi ya muda fulani

Dondoo: Chini

1. Rais wa kwanza wa Kenya 2. Tamka jina la Mungu 3. Mji mkuu wa Kenya 4. Fikiriwa 5.Ardhi ilimwayo 6. Ami 7. Vivyo hivyo 10.Wajibu wa kufanya jambo 12.Ujumbe usomwao mbele ya mgeni rasmi 13.mtutumuko wa maji 15. nyenyere 19.hutumia pesa aina ya Kwanza 21.Mtu mwenye elimu kubwa 22.Kinga 24.Mji Senegali 25.Pesa inayotumika India 26.Tengeneza 30. Fahamu

## Jibu Na: 9

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | O | G | O | T | A | ■ | ■ | M | A | M | B | O |
| A | ■ | H | ■ | H | I | T | L | E | R | ■ | A | ■ |
| T | H | A | M | A | N | I | ■ | A | U | N | I | A |
| I | ■ | R | A | M | A | N | I | ■ | S | ■ | N | ■ |
| L | A | I | N | I | ■ | G | | U | H | A | I | ■ |
| I | ■ | K | A | N | D | A | N | D | A | ■ | S | ■ |
| S | H | A | T | I | ■ | T | ■ | H | ■ | ■ | H | ■ |
| H | A | K | I | ■ | K | I | B | A | N | D | A | ■ |
| A | B | U | ■ | M | ■ | N | ■ | M | ■ | H | ■ | P |
| ■ | A | U | T | A | ■ | G | H | I | L | I | B | A |
| ■ | B | ■ | ■ | N | ■ | A | ■ | N | U | K | U | U |
| K | I | R | A | G | O | ■ | S | I | R | I | B | A |
| ■ | ■ | ■ | ■ | I | ■ | ■ | ■ | ■ | I | ■ | U | ■ |

# Darasa la ubora TBS lilivyong'arisha tija ya mzalishaji aliyetwaa leseni

**Na Sabato Kasika**

ILI kupata tija ya kibiashara duniani, moja ya hitaji kuu ni kuwa na ubora. Hicho ni kigezo muhimu kinachofuatiliwa kwa karibu na mamlaka za kibiashara katika nchi zote duniani, vivyo hivyo kinaangukia katika usimamizi wa ubora na wasimamizi wa kimataifa.

Hilo linafanya uendeshaji biashara duniani unakua na dai kukidhi ubora ndani na nje ya nchi. Nchini, kuna msimamizi mkuu ni Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Pia, kuna vyombo vingine vinavyosimamia ubora wa bidhaa sokoni kama Tume ya Ushindani (FCC) na inaelezwa kuna mambo muhimu wanayowajibika nayo wafanya biashara, ili kufikia mafanikio ya ubora unaokubalika.

Wataalamu wa biashara na ujasiriamali nchini wamekuwa wakifundishwa kuwa ni lazima mfanyabiashara wajiulize swali la msingi "nazalisha bidhaa zake kwa ajili ya nani?"

Nchini, inasisitizwa uzalishaji uwe na viwango vinavyokidhi kupata vyeti na leseni za ubora zinazotolewa (TBS).

Hicho kimekuwa kigezo muhimu kwa baadhi ya wafanyabiashara nchini wamekuwa wakijitahidi kutengeneza bidhaa zinazokidhi viwango na kutunukiwa vyeti vya leseni za ubora, kama njia ya kutambua huduma wanazozitoa.

Leseni TBS

Hivi karibuni TBS ilitunuku vyeti na leseni za ubora kwa baadhi ya wafanyabiashara, ambazo sasa zitatambulika kitaifa na kimataifa kwa kuweka nembo ya TBS, inayoashiria ubora na usalama wa bidhaa husika.

Katika tukio hilo, TBS ilitunuku leseni 75 za ubora, vyeti vya ubora 12 na cheti kimoja cha mfumo wa kusimamia usalama wa chakula (HACCP).

Pia ilitoa leseni endelevu zinazotolewa kwa wazalishaji wakubwa, wa kati na wadogo.

Kaimu Mkurugenzi wa Ubora wa TBS, Lazaro Msasalaga, anasema ni aibu iwapo mfanyabiashara atakiuka matakwa ya ubora akiwa na cheti na leseni za chombo hicho, huku akikiuka wasifu aliyotunukiwa.

Anasema, hiyo inamhahatarisha kunyang'anywa leseni au cheti alichopewa, kwa bidhaa zake kuharibiwa na ama kutozwa faini au kuondolewa sokoni.

"Hii ni hasara ambayo menejimenti ya TBS isingependa kuona inatokea. Tuna jukumu la kusimamia na kuandaa viwango vya kitaifa ili kuhakikisha maslahi ya nchi yanazingatiwa hata kikanda na kimataifa," anasema Msasalaga.

Mkurugenzi huyo anataja maeneo mengine ya viwango yanayoisimiwa na TBS ni: Utekelezaji wa viwango; kulinda afya na usalama wa walaji; kuongeza pato la taifa; na ukuaji uchumi wa viwanda.

Mdhibiti ubora huyo wa TBS, anawasisitizia wajasiriamali kusimamia ubora wa bidhaa zao, ili kuziongezea thamani zaidi sokoni, kwani shughuli hizo ni lango la ajira kwa Watanzania wengi na uchumi wao.

"Hadi sasa wajasiriamali 300 nchini wameshapata leseni na kutumia alama ya ubora ya TBS kwenye bidhaa zao na kuzifanya zipenye kwenye masoko mbalimbali, yakiwamo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC)," anasema.

Mtazamo wake ni kwamba, hayo ni mafanikio makubwa kwa taifa katika malengo ya taifa ifikapo 2025 kuwa imejenga uchumi wenye nguvu, imara na wenye ushindani.

"Wafanyabiashara ambao vyeti vyao vimekwisha muda wake waende ofisi za karibu za shirika letu (TBS), ili wapewe barua ya kielelezo kwa ajili ya kutumia kipindi cha mpito hadi leseni na vyeti vyao zitakapokuwa tayari," anasema.

Msasalaga anasema kwa sasa TBS imeongezewa majukumu ya kusimamia usalama katika machinjio, bucha, mama lishe na hoteli, vyote vitaendelea kufanya kazi wakati hatua za kuweka utaratibu mpya chini ya shirika hilo zinaendelea.



Kaimu Mkurugenzi wa Ubora wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Lazaro Msasalaga, akimtunuku leseni za kutumia alama ya ubora na vyeti vya ubora, Meneja Mauzo na Masoko Lake Lubes, Anil Gaur katika halfa ya utoaji wa leseni za biashara iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

**ALIYEFANIKIWA ANENA**

Katika orodha ya waliofanikiwa ni kampuni ya kuzalisha vilainishi vya mitambo mbalimbali, ikiwamo kwenye magari, Lake Lubes ya jijini Dar es Salaam. Anasema, mwaka jana walitunukiwa leseni moja, kisha zikafuata mbili, mara ya tatu wakapata tena mbili na sasa mara ya nne wametunukiwa vyeti vitatu leseni moja.

Mkuu wa Kitengo cha Mauzo na Masoko, Anil Gaur, anasema, sasa ni mara ya nne, huku akifafanua siri ya mafanikio katika vigezo kadhaa.

Anatamka mafanikio katika uzalishaji wa bidhaa bora yanatokana na kuzingatia vigezo anavyovifafanua:

"Siri kubwa ya mafanikio yetu katika uzalishaji wa bidhaa zenye ubora ni kuzingatia maelekezo ya TBS. Wao wanataka kabla ya kuzalisha bidhaa, mzalishaji anatakiwa kutuma maombi ya kukaguliwa bidhaa anayotaka kuzalisha.

"Sisi tumekuwa tukifanya kila tunapotaka kuzalisha bidhaa mpya, huwa tunatuma maombi kwao na wao wanawatuma wataalamu wao kuja kukagua na kuchukua sampo kwenda kupima bidhaa tunayotaka kuzalisha katika maabara zao kuona kama imekidhi viwango.

"Wakiona inakidhi, wanaturuhusu tuendelee kuzalisha na kuiingiza sokoni, lakini kama haina viwango au viwango viko juu, wanatoa ushauri kwamba tuongeze au tupunguze viwango, hivyo kwa utaratibu huo tumekuwa tukizalisha bidhaa zenye viwango."

"Sisi tulianza uzalishaji mwaka jana na tangu wakati huo tumetunukiwa leseni mbalimbali kulingana na bidhaa tunazozalisha kwani tumeshapata leseni," anasema Gaur.

"Kuendelea kutunukiwa leseni za ubora, ni hatua nzuri kwetu na tunaahidi kuendelea kuzalisha bidhaa kwa kuzingatia ubora, kwani hilo ndilo jambo la msingi la kuzingatia kama ambavyo TBS wanataka," anasema.

Gaur anasema, ni muhimu kwa kila mfanyabiashara ahakikishe bidhaa zake zinathibitishwa na TBS na wanalitambua hilo, ndio maana wamejikita zaidi kwenye ubora wa bidhaa zao.

Anakiri shirika lake linapata ushirikiano kwa Watanzania wengi, kwa sababu ya ubora wa bidhaa zao kwa kuwa na nembo ya TBS, na wanaongeza uzalishaji zaidi na kukuza soko. bora.

## HABARI KIMATAIFA

# Wahamiaji 150 wahofiwa kufa

**TRIPOLI,** Libya

ZAIDI ya wahamiaji 150 hawajulikani walipo baada ya boti walizokuwa wakisafiria kuzama kwenye pwani ya Libya katika Bahari ya Mediterania.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi, (UNHCR) pamoja na walinzi wa pwani nchini Libya walisema miongoni mwa wahamiaji hao ambao wanahofiwa wamekufa maji ni pamoja na wanawake na watoto.

Msemaji wa walinzi wa pwani ya Libya, Jenerali Ayoub Gassim, alisema boti mbili zilizokuwa zimewabeba wahamiaji wapatao 300 zilizama umbali wa kilomita 120 mashariki mwa mji mkuu wa Libya, Tripoli.

**Maofisa wetu walioko kwenye eneo la tukio wanawapatia msaada pamoja na huduma za matibabu.**

Alisema kiasi ya wahamiaji 137 wameokolewa na wamerejeshwa Libya na hadi sasa walinzi wa pwani wamefanikiwa kuupata mwili mmoja.

Msemaji wa UNHCR, Charlie Yaxley, alisema kuwa watu 147 wameokolewa hadi sasa na ameielezea ajali hiyo kama 'mbaya zaidi' kuwahi kutokea katika Bahari ya Mediterania kwa mwaka huu.

"Kundi la watu 300 liliondoka Khoms, Libya kwa boti. Tunaelewa kwamba walikuwa katika dhiki kubwa na awali waliokolewa na wavuvi wa eneo hilo na kisha na walinzi wa pwani ya Libya. Maofisa wetu walioko kwenye eneo la tukio wanawapatia msaada pamoja na huduma za matibabu," alifafanua Yaxley.

Yaxley alisema kwa mwaka huu mtu, mmoja alifariki akiwa njiani kutoka Libya kuelekea Ulaya kwa kila watu sita ambao walifanikiwa kufika katika mwambao wa Ulaya.

Mkuu wa UNHCR, Filippo Grandi, alisema hili ni janga baya kuwahi kutokea kwa mwaka huu. Katika ukurasa wake wa mtandao wa Twitter, Grandi, alizitaka nchi za Ulaya kurejesha shughuli za uokozi katika Bahari ya Mediterania, ambazo zilisitishwa baada ya uamuzi wa Umoja wa Ulaya na ametoa wito wa kumalizwa kwa suala la kuwashikilia wakimbizi na wahamiaji nchini Libya pamoja na kuongeza njia salama nje ya Libya.

Alisema hatua hizo zinapaswa kuchukuliwa sasa, kabla majanga zaidi hayajatokea. **DW**



Wahamiaji wakiwa kwenye kituo cha kuwashikilia wakimbizi cha Tripoli nchini Libya. **PICHA: REUTERS**

# Wanafunzi hoi baada ya kumgombea mwenzao

**KAMPALA,** Uganda

WANAFUNZI takribani 50 wa shule ya sekondari katika Wilaya ya Mbale Magharibi mwa Uganda , wamelazwa hospitalini baada ya kuvuta hewa ya gesi za kutoa machozi, limeripoti gazeti nchini humo -The monitor.

Wanafunzi hao walihusika katika mapigano yaliyoibuka baina ya shule za sekondari za Mbale Secondary school na Mbale High school kutokana na uhusiano wa kimapenzi.

Inadaiwa kuwa wakati wa ghasia hizo , polisi waliamua kufyatua mabomu ya kutoa machozi katika shule ya sekondari ya Mbale yaliyowaacha wanafunzi na walimu wao wakikimbia kwa ajili ya usalama wao.

Wanafunzi waliojeruhiwa wamelazwa katika hospitali ya rufaa ya Mbale , Joy Hospice, Viena Clinic, Mbale general clinic, miongoni mwa hospitali nyingine, limeeleza gazeti la The monitor.

Wanafunzi waliolazwa katika hospitali ya rufaa ya Mbale wanasema, mapigano hayo yaliibuka baada ya mwanafunzi kutoka shule ya sekondari ya Mbale kumvamia mwanafunzi wa Mbale high school, akimshutumu kumpenda mpenzi wake wa siku nyingi.

Msemaji wa kanda ya Elgon, Robert Tukei, alithibitisha tukio hilo lakini alipuuzilia mbali madai kuwa wanafunzi walilazwa kutokana na kuvuta hewa ya mabomu ya kutoa machozi.

"Polisi waliingilia kati kusitisha mapigano, yaliyokuwa yamezuka. Kama baadhi yao walijeruhiwa wakati wa mapigano, si lazima iwe ni kutokana na mabomu ya kutoa machozi ," alisema.

Tukei, hata hivyo alisema, wanafunzi 30 kutoka shule hizo mbili za sekondari wamekamatwa kwa kuchochea ghasia.

"Naweza kuthibitisha kuwa wanafunzi 30 wametiwa mbaroni kwa kuchochea ghasia na watashtakiwa ipasavyo ," alisema Tukei.

Washukiwa kwa sasa wanashikiliwa katika kituo kikuu cha polisi mjini Mbale. **BBC**

# Korea Kaskazini yaitishia Kusini



Makombora ya Pyongyang yaliyorushwa wiki hii. **PICHA: REUTERS.**

**PYONGYANG,** Korea Kaskazini

KOREA Kaskazini imetoa onyo kwa Korea Kusini kwamba ni vigumu kujilinda dhidi ya kombora lake jipya

Korea Kaskazini imetaja majaribio ya makombora yake mapya Alhamisi wiki hii kuwa onyo rasmi dhidi ya kile ilichokitaja kuwa uchokozi wa Korea Kusini.

Kombora hilo la masafa mafupi lilirushwa katika bahari ya Japan, pia ikijulikana kama bahari ya magharibi kutoka Wonsan katika pwani ya mashariki ya Korea Kaskazini.

Kiongozi wa taifa hilo Kim Jong Un, alisema kuwa taifa lake lililazimika kuunda silaha ili kukabiliana na tishio la moja kWa moja.

Alisema kuwa jaribio hilo lilishirikisha mfumo wa kiufundi wa kuelekeza makombora.

Matamshi ya Kim yaliyoripotiwa katika vyombo vya habari yanajiri baada ya Korea Kaskazini kukosoa uamuzi wa Korea Kusini na Marekani kushiriki katika zoezi la pamoja la kijeshi mwezi ujao.

Korea Kaskazini ilitaja zoezi hilo la kijeshi kama maandalizi ya kulivamia taifa hilo. Ijapokuwa Marekani na Korea Kusini zimekataa kufutilia mbali zoezi hilo la kila mwaka, wamepata pigo.

Mkuu wa Majeshi wa Korea kaskazini alisema kuwa moja ya kombora hilo lilisafiri kwa takriban kilomita 690 .

Marekani pia ilithibitisha kwamba makombora hayo ni ya masafa mafupi.

Rais Kim alisema kwamba ameridhishwa na mfumo huo wa kombora jipya na kudai kwamba haitakuwa rahisi kujilinda dhidi yake.

Korea Kusini imeitaka Pyongyang kuacha vitendo ambavyo havisaidii ili kupunguza hali ya wasiwasi na kusema kuwa majaribio hayo ni tishio la kijeshi.

Wizara ya Mambo ya Nje nchini Marekani imeitaka Korea Kaskazini kutofanya uchokozi.

Kwa mujibu wa mwanahabari wa BBC nchini Korea Kusini Laura Bicker, Pyongyang inailenga Korea Kusini kwa kutumia maneno na silaha.

Kombora hilo la masafa mafupi sasa linaweza kushambulia nchi yoyote ilio jirani na Pyongyang. Halafu kuna yale madai kwamba Korea Kusini ni ndumila kuwili - ikitafuta kuleta amani mbali na kununua silaha mpya na kushiriki katika zoezi la kijeshi la pamoja na Marekani.

Matamshi hayo huenda yakazua uhasama baada ya Rais wa Korea Kusini Moon Je, kufanya juhudi kubwa ya kuimarisha uhusiano kati yake na rais Kim Jong Un. **BBC**

# HADITHI

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina. Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

# JUMBA JEKUNDU- **11**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**




AMBALO walilokuwa hawajui Kadili na Meze ni kwamba nyumba ya tatu tu toka kwenye mti wa mwarobaini walipokuwa wameketo kwenye mawe makubwa ilikuwa ni ya mama Gombea.

Kwa mbali aliwaona wakati anapika. Kama kawaida yake, hakutaka kupitwa na kitu. Mapishi akamwachia binti yake Gombea na kujifanya anakwenda kwa jirani.

Akatembea kwa uangalifu hadi kwenye jumba lisiloisha. Akanyata na kunyata, akaambaa na ukuta hadi kwenye kona. Akawa na uwezo wa kuwachungulia bila wao kumuona kwa sababu walikuwa wamegeukia upande mwingine.

Alisikia kila kitu kilichokuwa kikizungumzwa. Na kuchanganya na yale aliyokuwa anayasikia kule dukani, alikafanikiwa kuunganisha mkasa mzima. Sasa ngoma ndiyo ikawa imempata mchezaji.

*****************************

Wakati mama Kadili akitwanga kisamvu chake, kwa mbali alimuona mama Gombea anakuja akiwa na mfuko wake.

"Bibi wewe mbona umetokea huku badala ya nyumbani kwako, au ulinipita hapa hapa?" Mama Kadili aliuliza kwa mashangao.

"Nilipita hapa asubuhi ulikuwa ndani sikutaka kukushtua, mwenzangu nakopesha vijora, ndiyo maana nilikuwa nazunguka huko kwa kina mama Pendo, mama Chilambo, na kwingine."

"Biashara hiyo mama Gombea umeianza lini?"

"Ndiyo naianza hivyo shoga 'angu hebu niunge mkono basi."

"Na kweli hiyo biashara mama Gombea inakufaa maana kwa kutembea wewe." alimtania na kumjibu swali lake.

"Nikope nitalipa nini ndugu yangu, hali yangu ya mkunga, nikijikuna natoka unga, nitaweza kulipa mimi?" Alijibu na kuuliza kwa pamoja.

"Mmmh mama Kadili, binti zako wawili wanakuuzia chakula unashindwa kukopa vijora kweli?"

"Nina michezo huyo shoga yangu, inanitia wazimu. Kwanza kwa mama Mtupeni nina mchezo, nimeingia majina matatu.

Kwa mama Shukuru nina majina mawili. Kwa mama Tabia nina jina moja. Huko kote kila siku pesa inatakiwa, we acha shoga kwanza nikalize halafu tutaangalia huko baadaye."

"Vipi shoga yangu, Kadili yupo?" Aliuliza mama Gombea kwa sauti ya chini.

"Na wewe mama Gombea, yaani kila ukija hapa lazima umuulize mwanangu, mna agenda gani huyu mwana."

"Aka mwaya, sina agenda yoyote, ila yale ambayo huwa nakwambia yamekuwa moto shoga yangu."

"Yapi tena hayo?"

"Si niliwahi kumwambia kuwa mwanao na rafiki yake Meze huwa wanakwenda disco na huko nikamwambia kuna siku unaweza kuletewa mkwe, tena toka familia tajiri?"

"Eee kweli nakumbuka."

"Sasa mambo yamekuwa mambo shoga yangu, ngoja nikusaidia kutwanga kisamvu kwanza kiive, tukae chini nikuhabarishe kabla mwenyewe hajaja."

"Hivi Kadili uko sawa kweli wewe?" Mama Kadili alimuuliza mwanaye wakati anakaribia kumaliza chakula.

"Ndiyo mama niko sawa."

"Hapana. Kuna kipindi hukuwa sawa, lakini baadaye ukabadilika nikaanza kukuona mwanangu umechangamka kama umetiwa ndimu, lakini siku hizi tatu nne naona kama una mawazo kama umefukuzwa kazi, yaani mpaka umenyorodoka, una nini mwanangu, unaumwa?"

"Siumwi mama niko sawa tu, maisha tu." Kadili alijibu, lakini alijua kuna jambo mama yake ameshalipata.

"Maisha gani yanayokufanya wewe uwe nyoro nyoro, hufanyi kazi, kila kitu mimi mama yanko na dada zako, wewe tumekuteua usome mpaka utakaposema basi ili uwe mkombozi wetu hapo baadaye. Hununui unga hununui sukari, shida nini mwanangu?"

Kadili alibaki kimya akimuangalia mama yake kana kwamba ndiyo anamuona kwa mara ya kwanza.

"Sikiliza mwanangu. Achana na mambo hayo, wewe soma utayakuta mbele." Maneno hayo yalimshtua Kadili alijiuliza ni kitu gani ambacho mama yake anaamisha.

"Habari zako zote ziko hapa, leo ngoja nikupasulie. Unapokwenda huko disco kuna mwanamke huko nasikia unakuwa naye. Lakini safari hii ya mwisho mlipoenda alikuja na mabaunsa wanamlinda na kuwatafuta wale wanaocheza naye ili wawapige. Kwa bahati nzuri yule mwanamke hakuwataja, ndiyo ikawa pone pone yenu."

> **Habari zako zote ziko hapa, leo ngoja nikupasulie. Unapokwenda huko disco kuna mwanamke huko nasikia unakuwa naye. Lakini safari hii ya mwisho mlipoenda alikuja na mabaunsa wanamlinda na kuwatafuta wale wanaocheza naye ili wawapige.**

Maelezo hayo yalimshtuka mno Kadili. Mbali na kushangaa mama yake kujua kila kitu, lakini pia mshangao mwingine ni jinsi habari nzima ilimvimfikia kwa kupindishwapindishwa.

Kuna kweli ndani yake, lakini si kwa jinsi mama yake alivyohadithiwa. Hakujua ni nani aliyekwenda kuongea umbea huo.

Walibadilisha eneo la mazungumzo kutoka dukani ambako walikuwa na wasiwasi napo kuwa siri zao zinavuja, lakini kule walikokwenda nako vile vile. Zimemfikia tena mama yake, tena zikaongezewa na chumvi juu.

"Sikiliza mwanangu, hao ni wanawake wa kupita. Hata ikiwa vipi huwezi kumpata msichana tajiri ukawa naye milele. Huwezi kumuoa. Unachoweza kufanikiwa ni kuwa naye tu kwa muda mfupi kwa sababu ya matamanio. Wewe ni masikini, huwezi kuwa na binti tajiri na mkadumu kwa muda mrefu. Kama ni kweli msahau kabisa na achana naye huyo binti, angalia masomo yako, baadaye utakuja kupata msichana mzuri utamuoa." Mama alitoa wasaa.

Kichwani mwa Kadili ulikuwa ni wasaa mzuri. Ni kweli hata yeye tayari alishaamua kuachana na mawazo hayo, ikiwa hata kwenda tena disco kule 'Blue Star'. Kwa sababu hata wakienda, tayari msichana huyo alisema hatokwenda tena hapo kwa sababu amebadilishiwa.

Aliwaza kuwa pamoja na yote hayo, mama yake ameshindwa kuelewa kuwa yeye na msichana huyo Edina walichoishia ni kucheza muziki tu na hakuna hata mmoja kati yao aliyewahi kuongelewa suala la mapenzi juu yao, japo ni kweli alitokea kumpenda.

"Mama nimekuelewa. Sitaki kusema zaidi. Lakini wewe ni mama yangu nafuata ushauri wako." Alijibu huku akiwa amejiinamia.

**Itaendelelea Jumamosi**

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

## ILANI

**TANZANIA PROTEINS CORPORATION LIMITED**

Inatolewa ilani kwa watu wote kwamba kampuni tajwa hapo juu iko mbioni kufutwa kwa ridhaa yetu.

**Wanahisa.**

115343902

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**AHMET BOZDEMIR** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE **NO T661 CKS.** ENGINE **NO CR 121542.** CHASSIS NO AK **12184243.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI **ARU/ARU /RB / 160335/2019.**

115344302$

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**BEATRICE E. MVUNGWA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 377** BSE AINA YA KING LION CHASSIS NAMBA **LTBPK8BG3G1K18808.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MWJ/RB/J790/2018.**

115343402

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**SHUFAA ABUSHIRI KOSHUMA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI (GUTA) YENYE NO **T428 BSS.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **ARU/RB /160481/2019. AU PIGA SIMU 0752 631 878.**

115343002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA MBEYA**

**SHAURI LA MADAI YA RUFAA NO.8/2016**

**ERASTO KAMALA MWAMBUSYE..................MDAI**

**DHIDI YA**

**JUBILEE INSURANCE CO.LTD............MRUFANI WA KWANZA**
**CABLE TELEVISION NETWORK............MRUFANIWA WA PILI**

**Kwa : 1.CABLE TELEVISION NETWORK,PO POTE ULIPO TANZANIA.**

**KUITWA SHAURINI**

Unaamriwa na Mahakama hii uhudhurie hapa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya tarehe 29/08/2019 siku ya Alhamisi Saa 3.00 asubuhi,ambapo shauri limepangwa kusikilizwa.

ELEWA KWAMBA Ukikosa kufika siku hiyo shauri litasikilizwa bila wewe kuwepo na uamuzi kutolewa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 26 Mwezi Julai, 2019.

115344002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO MPANDA - KATAVI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo: MPANDA- KATAVI**

**Usimamizi wa Mirathi No. 56/2011**

**Ombi la ERNEST DAVID kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu DAVID MUHALURO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 1/8/2019. kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 25/7/2019.

E. M TALLANGYO

115343102

**MAHAKAMA YA WILAYA MOROGORO**

**MAOMBI NAMBA 06 YA MWAKA 2019**

**NARSIS BONY SHAO.....................MWOMBAJI**

**Dhidi ya**

**CHRISTINA BERTIN MUSHI...........MJIBU MAOMBI**

**TANGAZO;**

Mjibu maombi tajwa hapo juu unatakiwa kufika mbele ya mahakama hii ya watoto,Mahakama ya mwanzo Mjini Morogoro(NUNGE),Tarehe 01/08/2019 Saa 2:30 asubuhi bila kukosa.

Mjibu maombi ,usipofika mahakamani siku hiyo shauri litatajwa na kuendelea kusikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo mahakamani na kutolewa uamuzi.

Amri hii imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 25 mwezi 07 mwaka 2019.

215343202

## TANGAZO TANGAZO SAW MILL INAUZWA

ONE CIRCULAR SAW MACHINE TYPE-J152 – (MOBILE) PERKING DIESEL INGENE 90 HP INAPASUA MBAO NGUMU NA LAINI MISUMENO YAKE IPO

**MAWASILIANO:- 0754 090 021 , 0754 845 669.**

215342702

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311***

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Fernandez njia nyeupe Man United

**LISBON,** Ureno

KOCHA wa Sporting CP, Marcel Keizer, amesema kuwa mchezaji wake, Bruno Fernandez anaweza kujiunga na Manchester United.

Kiungo huyo alikuwa kwenye rada za United kabla ya Keizer kusema kuwa hawezi kumwachia kwa kuwa yupo kwenye mipango yake.

"Kila mmoja angependa abakie ndani ya timu kutokana na uwezo wake na msaada anaoutoa ndani ya timu, ila kwa sasa hatujui kitakachotokea mbele ni jambo la kusubiri na kuona," alisema.

Ameongeza kuwa kwa sasa kuna uwezekano mkubwa wa mchezaji huyo kujiunga na United, kwa sababu hataweza tena kumzuia.

"Nilikuwa nataka abakie hapa, lakini ni wazi kwamba naona hatutakuwa na uwezo wa kumbakisha, naamini anaweza kwenda United."

Dau la nyota huyo linatajwa kuwa ni pauni milioni 62, hivyo United wakiweka mezani kitita hicho, watampata kiungo huyo, ambaye amefunga mabao 20 katika mechi 30 za mashindano yote na kutengeneza nafasi za magoli 13.





# LINDELOF: SIMHOFII MAGUIRE

**RIO DE JANEIRO,** Brazil

BEKI Victor Lindelof amesema yuko tayari kwa vita ya namba kikosini dhidi ya Harry Maguire kama dili lake la kutua Manchester United litakamilika.

Ofa mbili za United kwa ajili ya beki huyo wa kati wa Leicester zimeshakataliwa huku klabu yake ikisimamia kutaka dau la pauni milioni 90.

Lindelof tayari yuko katika vita ya namba dhidi ya Eric Bailly, Phil Jones na Chris Smalling, huku watu kama Marcos Rojo na Axel Tuanzebe nao pia wakitolea macho nafasi hiyo.

"Napenda ushindani," Lindelof alisema. "Hakika naupenda. Nadhani ni jambo zuri kwa klabu kuwapo kwa ushindani.

Ukiwa na wachezaji wazuri katika nafasi yako unalazimika kufanya kazi kwa juhudi zaidi kila siku, hasa mazoezini, na hilo linaisaidia timu kwenda kwenye nafasi za juu zaidi," alisema.

"Sidhani kama ushindani wa namba ni tatizo kwangu, kwani nina uhakika nitaweza kupambana naye na hatimaye kubakia kwenye kikosi cha kwanza," alisema.

# *Kamari yamponza Yerry Mina*

**LONDON,** England

BEKI wa Everton, Yerry Mina, amefunguliwa mashtaka ya kisoka na FA ya England baada ya kutokea katika tangazo la kamari kwao Colombia kitu ambacho ni kinyume na kanuni za soka la nchi hiyo, ingawaje klabu yake inatangaza kamari.

Mina amepewa mpaka siku ya leo kujibu mashtaka hayo na taarifa ya FA ilisikika ikisema. "Yerry Mina wa Everton amefunguliwa mashtaka kutokana na kanuni za suala la kamari za FA.

Inaaminika beki huyo alivunja kanuni E8 [3] kwa kushiriki katika tangazo la kamari ambalo amepigwa marufuku kufanya hivyo."

Mina mwenye umri wa miaka 24 mpaka sasa bado hajajiunga katika kikosi cha Kocha Marco Silva kufuatia ushiriki wake katika michuano ya Kombe la Mataifa ya Amerika Kusini, Copa Amerika, huku likizo yake ikiwa imeongezwa muda.



## HABARI MICHEZO

# GUARDIOLA: SITAKI KUMPOTEZA SANE



**SHANGHAI,** China

KOCHA Pep Guardiola amesema kuwa anamtaka Leroy Sane kubakia Manchester City, lakini amekiri kwamba uamuzi huo hauko mikononi mwake.

Sane mwenye umri wa miaka 23 ana miaka miwili iliosalia katika mkataba wake lakini bado hajaanza mazungumzo ya kuongeza mkataba mpya.

Winga huyo wa Ujerumani alifunga mabao mawili katika mechi ya ushindi dhidi ya timu ya Hong Kong Kitchee katika mchezo wa kirafiki hivi karibuni ukiwa ni wa maandalizi ya msimu ujao, huku David Silva , Raheem Sterling na kinda wa Hispania, Nabil Touaizi pamoja na Iker Pozo wakifunga.

"Tunamtaka abakie na kuna ofa inayosubiri ya kuongeza mkataba wake," alisema Guradiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Hatima yake haipo mikononi mwetu, akiamua kuondoka anaweza kuondoka. Iwapo anataka kuondoka anaweza kufanya hivyo lakini hatutafurahia."

Mapema wiki hii Guardola alinukuliwa akisema kwamba, anataka wachezaji wote kuwa na furaha ndani ya City na mchezaji ambaye ataona hapamfai anaweza kuruhusiwa kuondoka.

# *Ozil, Kolasinac wavamiwa na majambazi*

**LONDON,** England

WACHEZAJI wa Arsenal, Mesut Ozil na Sead Kolasinac wameripotiwa kuvamiwa na genge la majambazi katika jaribio la wizi wa gari katika barabara za mji wa London, England.

Klabu ya Arsenal imethibitisha kuwa wachezaji wake Ozil na Kolasinac walilengwa na majambazi hao waliokua wamejihami, lakini hawakujeruhiwa katika tukio hilo.

Katika taarifa yake Arsenal imesema: "Tumewasiliana nao na wachezaji wote wawili wako salama."

Kanda ya video iliyosambazwa kwenye mitandao ya kijamii inamuonyesha Kolasinac akipigana na na wanaume wawili waliokuwa wamejihami kwa visu. Mchezaji huyo pia anaonekana akiruka kutoka kwenye gari kukabiliana na wanaume waliokuwa wameficha nyuso zao na ambao walikuwa na njama ya kuwaibia.

Msemaji wa polisi wa jiji la London amesema: "Tumepata taarifa kuwa washukiwa waliokuwa juu ya pikipiki walijaribu kumuibua mtu aliyekuwa akiendesha gari.

"Dereva pamoja na abiria wake walifanikiwa kuondoka eneo la tukio bila kujeruhiwa na kwenda hadi eneo la Golders Green, ambako wamewasilisha taarifa kwa maafisa wetu."

Hakuna mshukiwa yeyote aliyekamatwa kufikia sasa .

Kolasinac na Ozil ni wachezaji wa kwanza wa soka kuvamiwa katika barabara za London.



# Bondia wa Argentina afariki baada ya kipigo

**BUENOS ARIES,** Argentina

BONDIA wa Argentina, Hugo Santillan, amefariki dunia kutokana na majeraha aliyopata katika pambano, ikiwa ni siku chache baada ya kifo cha bondia wa Urusi, Maxim Dadashev.

Bondia huyo mwenye umri wa miaka 23 alizirai ukumbini siku ya Jumamosi iliyopita, baada ya pigano lake la kuwania mkanda wa WBC dhidi ya Eduardo Javier Abreu wa Argentina kumalizika kwa sare.

Alipelekwa hospitalini na kufanyiwa upasuaji lakini akafariki siku ya Alhamisi.

Santillan ni bondia wa pili kufariki kutokana na majeraha aliyopata katika ulingo wa ndondi wiki hii baada ya kifo cha Dadashev kuthibitishwa siku ya Jumanne.

Bondia huyo mwenye umri wa miaka 28 alipelekwa hospitalini akitokwa na damu katika ubongo baada ya pigano lake la kuwania mkanda wa IBF uzito wa Welter dhidi ya Subriel Matias kusimamishwa mwisho wa raundi ya 11 Ijumaa iliopita.

Alifanyiwa upasuaji wa dharura lakini ukashindikana na kusababisha kifo chake.

Bondia huyo wa Urusi aliondoka uliongoni kwa kubebwa kwenye machela na kukimbizwa hospitalini, lakini jitihada za madaktari hazikuzaa matunda.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KLABU NNE ULAYA ZAMWANIA PEPE

## Napoli inatajwa kuwa katika nafasi nzuri ya kunasa saini ya winga huyo...

**LILLE,** Ufaransa

RAIS wa Lille, Gerard Lopez, amethibitisha kuwa amepokea ofa kutoka katika klabu nne tofauti, zote zikitaka kumsajili Nicolas Pepe.

**Lopez alizitaja klabu hizo kuwa ni pamoja na Arsenal na Liverpool ambazo zote zimekubali kutoa kiasi cha pauni milioni 71.7, ambazo zimetajwa katika mkataba wa nyota huyo.**

Timu mbalimbali barani Ulaya zimeonyesha nia ya kumsajili Pepe kutokana na kuonyesha kiwango bora katika msimu uliomalizika akiwa na Lille, ambayo imefanikiwa kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao, baada ya kumaliza katika nafasi ya pili nyuma ya mabingwa Paris Saint-Germain kwenye Ligue 1.

Lopez alithibitisha katika mahojiano maalumu na Tuttosport kuwa klabu nne zimefikia makubaliano ya kulipa dau lililotajwa la kumsajili winga huyo, wakati L'Equipe iliandika kuwa klabu hizo nne zinazomwania nyota huyo ni pamoja na Napoli, Liverpool, Arsenal na Inter.

"Tumepokea ofa ambazo zimekubali kutoa kiasi cha fedha tulichosema na ni klabu kubwa," alisema Lopez, alipokuwa anahojiwa na Gianluca Di Marzio.

"Napoli iliwasilisha ofa kwa ajili ya kumsajili Pepe na ilifikia malengo yetu ya kulipa Euro milioni 80.

"Sasa ni jukumu la mchezaji mwenyewe kufanya uamuzi ni klabu ipi atataka kwenda kuitumikia kutokana na ofa ambazo wakala wake alikuwa anazifanyia kazi za klabu zote nne.

"Pepe anatarajia kurejea klabuni Jumatatu baada ya kumaliza mapumziko yake na ninafiriki hadi kufikia katikati ya wiki ijayo, atakuwa ameshafanya uamuzi ni klabu ipi ataichagua."

Taarifa kutoka kwa watu wa karibu na Pepe zinasema kuwa nyota huyo ana nafasi kubwa ya kujiunga na Napoli na kuziacha timu nyingine tatu zilizokuwa zikimwania pia.

Inaelezwa pia wakala wake amekutana na mabosi wa klabu ya Serie A ili kuhakikisha wanakamilisha mchakato huo wa usajili, huku wakijiandaa kumtoa mshambuliaji wao, Adam Ounas ili kukamilisha usajili huo.

## ZISIKUPITE

### EVERTON YAITEGA PALACE

EVERTON imeieleza Crystal Palace kuwa inajiandaa kutoa pauni milioni 60 pamoja na straika Mturuki Cenk Tosun, kama sehemu ya usajili wa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Wilfried Zaha, lakini bado inahofia itamkosa nyota huyo. ***(Telegraph)***

### SPURS KUFANYA KWELI

MWENYEKITI wa Tottenham, Daniel Levy, amemweleza Kocha Mauricio Pochettino kuwa atahakikisha anampa fungu la kutosha kwa ajili ya kufanya usajili baada ya kupata udhamini wa pauni milioni 320, tayari klabu hiyo imewasilisha ofa ya kumwania mshambuliaji wa Juventus, Paulo Dybala (25). ***(The Times)***

### MAGUIRE KUIKAMUA UNITED

MANCHESTER United italazimika kutoa kiasi cha pauni milioni 80 kinachotakiwa na Leicester City ili kumnasa beki wa Timu ya Taifa ya England, Harry Maguire baada ya beki wake wa kati, Eric Bailly (25) kupata majeraha katika mguu kwenye mchezo wa kirafiki uliochezwa juzi dhidi ya Tottenham. ***(Mirror)***

### VALLEJO KUTUA WOLVES

WOLVES wako katika mazungumzo ya kumsajili beki wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Vijana ya Hispania ya umri chini ya miaka 21, Jesus Vallejo (22), kwa mkopo wa muda mrefu, huku pia ikikaribia kukamilisha mchakato wa kumwania straika wa AC Milan Mtaliano Patrick Cutrone (21) ambaye dau lake ni pauni milioni 17. ***(Mail)***

### SOARES AWEKWA SOKONI

BEKI wa Southampton Mreno Cedric Soares (27), anawindwa na Monaco huku Ralph Hasenhuttl akijipanga kupunguza kiasi cha mshahara anaolipwa kwenye klabu hiyo. ***(Foot Mercato)***

### THAMANI YA TOBY YAONGEZEKA

THAMANI ya beki wa Spurs, Toby Alderweireld imeongezeka baada ya muda uliotajwa kwenye mkataba wake kumalizika tangu juzi. Thamani iliyokuwa kwenye mkataba wa beki huyo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji ambayo sasa itapanda ilikuwa ni pauni milioni 25. ***(Sun)***

### SERGEJ AKARIBIA UNITED

MANCHESTER United inajiandaa kumkosa kiungo wake Mfaransa Paul Pogba (26) ambaye anaondoka klabuni hapo na yenyewe ikiwa katika hatua za mwisho za kukamilisha mchakato wa kumsajili nyota wa Timu ya Taifa ya Serbia na Lazio, Sergej Milinkovic-Savic (24), kwa dau la pauni milioni 70. ***(Mirror)***

### NAKAMBA KUTUA VILLA

ASTON Villa iko katika hatua za mwisho za kukamilisha usajili wa mchezaji wa 11 katika kipindi hiki cha majira ya joto, ikiwa imeshatumia kiasi cha pauni milioni 120 na kumtaja Marvelous Nakamba wa Club Brugge. ***(Telegraph)***

### MALCOM ANUKIA DORTMUND

MABOSI wa Borussia Dortmund wako katika mazungumzo ya kumsajili mshambuliaji wa Barcelona Mbrazil, Malcom kwa dau la pauni milioni 37.5. ***(Goal)***

### LONGSTAFF KUIKAMUA UTD

MANCHESTER United imeambiwa ijiandae kutumia zaidi ya pauni milioni 30 ili kumsajili kiungo wa Newcastle, Sean Longstaff, ambaye ana umri wa miaka 21 na ni raia wa England. ***(Manchester Evening News)***

# MAMA SAMIA AAHIDI MAKUBWA

**Na Shufaa Lyimo**

MAKAMU wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan na Mlezi wa Shirikisho la Michezo ya Mashirika ya Umma, Taasisi na Kampuni Binafsi (SHIMUTA), amesema atahakikisha anashirikiana na serikali kuboresha miundo mbinu ya viwanja vya michezo ili kumaliza changamoto hiyo inayowasumbua wanamichezo mbalimbali nchini.

**Mama Samia alisema hayo jana, wakati alipokuwa anazungumza na wadau mbalimbali wa michezo ili kujadili sababu ambazo zimelifanya shirikisho hilo kudorora tofauti na ikilinganishwa na miaka iliyopita.**

Alisema changamoto hiyo ya miundombinu imekuwa kubwa hali ambayo amekiri kuifanyia kazi kwa kushirikiana na viongozi wa taasisi mbalimbali ili kuhakikisha malengo ya Shimuta kusonga mbele yanatimia.

"Changamoto ya miundombinu ya viwanja inaonekana kuwa kubwa kwa sababu kila mdau ameizungumzia, mimi kama mlezi wa Shimuta nitatekeleza ilani ya chama changu kilichonipa madaraka, nitafanya kazi ya kusimamia michezo pamoja na utamaduni," alisema Mama Samia.

Hata hivyo kiongozi huyo alisema kuwa anasikitishwa kuona Shimuta inashindwa na vyama vingine vinavyosimamia mashindano yanayoshirikisha wanafunzi na kuongeza kwamba wanataka kuona michezo yao inarejea kwa kasi ili lengo la kuimarisha afya za wafanyakazi kupitia michezo liweze kutimia.

"Hali iliyopo Shimuta kwa sasa hairidhishi, tunashindwa na mashindano ya shule, miaka ya sasa kukiwa na mashindano hakuna watu uwanjani, nasisitiza wafanyakazi wote watambue kuwa michezo inaleta mahusiano mazuri, ninaahidi kutekeleza yote yaliyojadiliwa katika mkutano huu," Mama Samia alisema.

Kiongozi huyo alimpongeza Mwenyekiti wa Shimuta na kamati yake kwa kulitumikia vema shirikisho hilo, na kudai anataka mwaka huu timu ziongezeke katika mashindano ambayo yatafanyika Novemba jijini Mwanza.

"Timu zikiongezeka kwenye mashindano ya Mwanza nitashirikiana na nyie, endapo kama zitakuwa chini ya timu 30 sitakuja, nitamtuma mwakilishi wangu kwa sababu kutakuwa hakuna kilichobadilika," aliongeza.

Naye Mwenyekiti wa shirikisho hilo, Khamis Mkanachi, alisema kuwa anamshukuru mlezi huyo kwa kuendelea kushirikiana nao bega kwa bega tangu alipoingia madarakani na kumwahidi idadi ya timu zitakazoshiriki katika mashindano ya mwaka huu itaongezeka.

"Sisi kama Shimuta, tutahakikisha tunazidi kulitangaza shirikisho letu kwa kushirikiana na wadau wa michezo, ikiwa pamoja na kufanya bonanza kama ambavyo mlezi wetu alivyopendekeza," alisema Khamis.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Dar es Salaam, William Anangisye, alisema kwa upande wao wanakabiliwa na changamoto ya viwanja kwa kudai viwanja vilivyopo, havina hadhi ya kuchezea michezo ya Olimpiki.

Anangisye alisema mara nyingi wachezaji wanatamani kufanya mashindano makubwa lakini wanashindwa kutokana na uhaba wa miundombinu.

"Bila ushirikiano hakuna kitu tutakachokifanya, kila siku tutajiona tupo nyuma vile vile, huu ni wakati wa kuwapa vijana fursa ili tupunguze gharama za kutafuta wachezaji wengine wakati kuna vijana wenye vipaji vya kutosha," alisema Mwenyekiti wa Chama cha Netiboli Tanzania (Chaneta), Devota Minja.

## Bonanza la Utalii kufanyika Pemba

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WANAMICHEZO kutoka sehemu mbalimbali wanatarajia kushiriki katika Bonanza la Utalii na Michezo litakalofanyika kesho kwenye Uwanja wa Gombani, Pemba imeelezwa.

Ofisa Mdhamini wa Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Khatibu Juma Mjaja, alisema jana kuwa tamasha hilo litashirikisha michezo mbalimbali na wanamichezo watakaofanya vema watapata zawadi.

Mjaja alisema katika siku ya kwanza ya bonanza hilo kutakuwa na mashindano ya mbio za Nyika ambayo yataanza saa 2:00 asubuhi na hii itakuwa ni mara ya kwanza kwa mchezo huo kuchezwa kisiwani Pemba.

Alisema kuwa mbio hizo zitawajumuisha wanariadha kutoka maeneo tofauti hapa nchini pamoja na wenyeji wao wa Pemba ambao wamejiandaa vema kufanya vizuri katika mbio hizo.

## Dullah Mbabe, Kamata ulingoni

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA maarufu wa ngumi za kulipwa nchini, Abdallah Shabani maarufu Dula Mbabe na Paulo Kamata wanatarajia kupigana katika pambano la raundi 10 litakalofanyika leo kwenye Ukumbi wa Escape One jijini Dar es Salaam.

Mabondia hao jana walipima uzito na kujiweka tayari kwa pambano hilo linalotarajiwa kuwa na ushindani huku kila mmoja akitamba kumshinda mwenzake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa Dula Mbabe, Omary Pelege, alisema pambano hilo litakuwa la uzito usiopungua 75-76 na bondia wake amejiandaa kuendeleza rekodi nzuri ya kuwachapa wapinzani wake.

Aliongeza kuwa bondia wake yuko "fiti" kutokana na mazoezi ya muda mrefu aliyokuwa anampa katika kujiandaa na pambano hilo.




Mwandishi wa Habari za Michezo nchini, Gift Macha (wa pili kutoka kulia), akizungumza kwa niaba ya waandishi waliojitokeza kuiunga mkono Timu ya Taifa (Taifa Stars) inayojiandaa na mechi dhidi ya Kenya (Harambee Stars), ambayo itachezwa kesho kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# 'Mbio za Afcon' zamwaga zawadi

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019) zikiwa zimefikia ukingoni huko nchini Misri, baadhi ya wadau wa michezo wa hapa nchini walioshiriki kubashiri matokeo ya baadhi ya mechi bado wanajikuta wakibadilisha maisha yao kutokana na kuibuka washindi na kujinyakulia zawadi mbalimbali, imefahamika.

Fred Chacha, mkazi wa Geita, ameibuka mshindi wa shindano la 'Mbio za Afcon' lililokuwa likiendeshwa na Kampuni ya Kubashiri la Parimatch na kujipatia zawadi ya pikipiki mpya kabisa aina ya TVs.

Akizungumza wakati wa hafla ya utoaji zawadi kwa washindi wa shindano hilo jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mwendeshaji wa kampuni hiyo, Tumaini Maligana, alisema Watanzania 10 walipata bahati ya kuibuka na zawadi mbalimbali baada ya kubashiri matokeo kwenye mechi za michuano hiyo ya Afcon.

Maligana aliwataja washindi wengine wa shindano hilo kuwa ni Abdulaziz Said kutoka Mtwara na Joseph Kashinye wa Sumbawanga ambao walijipatia televisheni kubwa LG Smart inchi 43 na Sebastian Mwita wa Geita, Frank Mlinga (Shinyanga) na Siledius Bugasa wa Mwanza ambao walijipatia simu za mkononi aina ya Samsung A8+.

Washindi wengine wanne wa shindano hilo la Parimatch, Ally Nkwembe (Mtwara), Novatuis Chibuga (Iringa), Emmanuel Karama (Sumbawanga) na Aziz wa Mbeya walimalizia orodha ya washindi wakiwa wamejipatia simu za mkononi aina ya Samsung M20.

Mlinga akizungumzia kwa niaba ya wenzake alisema kuwa amefurahi kupata zawadi hiyo ambayo itasaidia kubadilisha maisha yake.

"Tunafuraha sana, baada ya kuambiwa tumeshinda, karibu kila mmoja hapa alipata mshtuko kusikia taarifa hii, wengine hatukujua kama tulikuwa tunawekwa katika shindano," alisema Mlinga.

Michezo
Jumamosi Julai 27, 2019
Nipashe



Lindelof: Simhofii Maguire UKURASA 28



Wachezaji wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), wakiwa kwenye mazoezi ya timu hiyo inayojiandaa kuwavaa Kenya (Harambee Stars), katika mechi itakayochezwa kesho jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# Bocco, Kaseja waula Stars

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI wa Simba, John Bocco, ameteuliwa kuwa nahodha wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), ambayo inajiandaa na mashindano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), imefahamika.

Taifa Stars iko kambini ikijiandaa na mechi dhidi ya majirani zao wa Kenya (Harambee Stars), itakayochezwa kesho na watarudiana Agosti 2 mwaka huu jijini Nairobi, Kenya.

Kaimu Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije, alisema kuwa Bocco ambaye pia ni nahodha wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, atasaidiana na golikipa mkongwe nchini, Juma Kaseja na mabeki, Kelvin Yondani na Erasto Nyoni.

"Hawa watakuwa viongozi kwa timu hii inayoshiriki mashindano ya CHAN," alisema Ndayiragije, ambaye amechukua mikoba iliyoachwa na Mnigeria Emmanuel Amunike.

Wakati huo huo, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Afrika (TFF), Clifford Ndimbo, alisema jana kuwa maandalizi ya mechi hiyo yamekamilika na mchezo huo utachezeshwa na waamuzi kutoka Burundi na walitarajiwa kuwasili nchini jana jioni.

Ndimbo aliwataja waamuzi hao kuwa ni pamoja na Tierre Nkurunzinza na atasaidiwa na Herve Kakunze pamoja na Paschal Ndimunzigo huku mwamuzi wa akiba akiwa ni Goerges Gotagota.

"Mechi itaanza saa 10:00 jioni, kiingilio cha chini kitakuwa ni Sh. 3,000, wakati VIP B na C itakuwa ni Sh. 5,000," alisema kiongozi huyo.

# Aussems: Watasubiri

## Atamba Simba itatetea ubingwa mapema, kuivaa Township Rollers leo...

**Na Somoe Ng'itu**

WATASUBIRI! Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, amesema kuwa kikosi chake kimeimarika na kiko tayari kwa ajili ya kuanza vita ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/20 pamoja na mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Aussems, alisema kuwa Kamati ya Usajili imetekeleza mapendekezo yake kwa zaidi ya asilimia 80 na anaamini ubora wa wachezaji alionayo, wapinzani wao wasitarajie kutwaa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara ambalo wanalishikilia.**

Aussems alisema kuwa ushindani ambao anauona kwenye mazoezi ya timu hiyo, unaonyesha kila mchezaji ana kiu ya mafanikio na kupambana kusaidia kutimiza malengo ya klabu hiyo.

"Timu yangu sasa iko katika nafasi nzuri, wachezaji wameimarika na kila mmoja anaonyesha yuko tayari kwa ajili ya kuanza msimu, tunahitaji kufanya vizuri, ndiyo maana tumekuja huku kuweka mambo sawa, naamini tutafikia malengo," alisema Aussems.

Aliongeza kuwa mechi za kirafiki ambazo wamecheza, zimewasaidia kuwaimarisha wachezaji na kufahamu upungufu wao, ambao ameufanyia kazi.

"Tumetengeneza kikosi bora kwa ajili ya msimu ujao, tunajua ligi haitakuwa nyepesi, kila timu imejiimarisha kwa sababu inataka kupata matokeo mazuri, sisi pia tumefanya hivyo, tumesajili wachezaji wapya ili kuongeza nguvu," Mbelgiji huyo alisema.

Naye Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema kuwa kikosi chake kimeendelea na programu zake za mazoezi na leo wanatarajia kucheza mchezo mwingine wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Township Rollers.

Alisema kuwa licha ya nyota wao saba kurejea nchini na kujiunga na kambi ya Timu ya Taifa (Taifa Stars), bado kikosi kilichobakia mjini Rustenburg ni imara na kila mmoja anaonyesha bidii kwenye mazoezi.

"Tumebaki na wachezaji 19, ila mazoezi yanakwenda vizuri kama kawaida, vijana wako tayari kwa ajili ya mechi nyingine ya kirafiki itakayochezwa kesho (leo) dhidi ya Township Rollers kuanzia saa 4 :00 asubuhi hapa, sawa na saa 5:00 asubuhi huko nyumbani," alisema Rweyemamu.

Baada ya kurejea nchini, mabingwa hao wa Bara wataanza kufanya shughuli mbalimbali za kijamii ambazo zitahitimishwa na Tamasha la Simba Day ambalo ni maalumu kwa kutambulisha wachezaji na jezi mpya.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002